# Nipashe

Jumatatu Aprili 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580548

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**Grealish kukaa tena nje wiki 2**

UKURASA 21

**Ripoti** ya CAG: Zitto aibuka na hoja za tril. 3.6/-

UKURASA 4



**CRDB** yatoa mil. 10/-, chakula kwa watoto wenye uhitaji

UKURASA 8

# Simulizi za Mbowe akaunti zake kufilisiwa

• **Asema** alikimbilia kuwekeza Dubai, Afrika Kusini...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**CAG: MIKOPO HESLB INAUMIZA WATUMISHI**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kuwapo kwa mikopo Iliyopindukia...

UKURASA WA 5

**SERIKALI YATOA BEI ELEKEZI RAMADHANI**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imetangaza bei elekezi kwa ajili ya bidhaa za vyakula vinavyotumiwa...


## Samia, Museveni waeleza fursa bomba la mafuta

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Yoweri Museveni wa Uganda, alipowasili katika Ikulu ya Entebbe kwa ziara ya kikazi ya siku moja jana. **PICHA: IKULU**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na familia yake, wakiwahudumia watoto chakula wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa futari iliyofanyika katika viwanja vya Karimjee. Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 10 umetolewa kwa vituo 10 vya watoto yatima vilivyopo Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya sadaka kuelekea mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Lissu aomba kuzungumza na Rais Samia

UKURASA 3







Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **MWAMBUSI AANIKA SABABU YA SARE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia, Museveni waeleza fursa bomba la mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

MARAIS Samia Suhulu Hassan wa Tanzania na Yoweri Museveni wa Uganda jana wameshuhudia utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji wa mradi ujenzi wa bomba mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kati ya serikali za nchi hizo na kampuni za uwekezaji uliofanyika katika Ikulu ya Entebbe nchini Uganda.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Samia alisema mradi huo utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi zote mbili kwa kuongeza mapato ya taifa, kuzalisha ajira, kukuza utangamano na kuinua ustawi wa jamii.

Rais Samia alitoa wito kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuendeleza jitihada za kuimarisha miundombinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege ili kuunga mkono uwekezaji huo pamoja na mwingine unaolenga kuimarisha uchumi na kuboresha maisha ya watu.

Alimhakikishia Rais Museveni kuwa serikali anayoiongoza itaendeleza na kukuza zaidi ushirikiano na uhusiano uliopo baina ya nchi hizo ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo mapya ya ushirikiano.

Kwa upande wake, Rais Museveni alimshukuru Rais Samia kwa kuitikia wito wake wa kwenda kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo na kufanya ziara yake ya kwanza nje ya nchi tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Museveni, alizungumzia manufaa mbalimbali yatakayopatikana katika mradi huo kwamba sio tu kwa Uganda na Tanzania bali pia Afrika Mashariki ambazo zitakuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta ya na kwa gharama nafuu.

Rais Museveni alisema sababu za kupitisha bomba hilo nchini Tanzania kuwa ni pamoja na kuwa na manufaa ya kiuchumi na pia kwa Uganda kutambua mchango wa Tanzania katika kumuondoa aliyekuwa mtawala wa nchi hiyo Nduli Idd Amin Dada na pia kama ndugu, jirani na rafiki wa kweli.

Kadhalika, utekelezaji wa mradi huo, Uganda utarahisisha mpango wake wa kununua gesi kutoka nchini Tanzania.

Hafla ya utiaji saini mikataba ya mradi huo imehudhuriwa na mawaziri na wawakilishi wa kampuni hizo za uwekezaji ambazo ni TOTAL ya nchini Ufaransa na CNOCC ya China.

Marais hao walishuhudia utiaji saini wa mkataba wa kwanza ambao ni wa uenyeji wa mradi kati ya Serikali ya Uganda na wawekezaji (TOTAL na CNOCC), mkataba wa pili ni wa ubia, Serikali za Tanzania na Uganda zimetiliana saini na kampuni hizo na mkataba wa tatu ni wa masuala ya kikodi na usafirishaji, Serikali ya Uganda imetiliana saini na kampuni hizo (TOTAL na CNOCC).

Pamoja na kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, marais pia walitia saini tamko la pamoja kuhusu utekelezaji wa mradi huo na kuagiza vipengele vilivyobaki katika utekelezaji vikamilishwe haraka.

Mradi huo utahusisha ujenzi wa bomba la mafuta litakalotumia teknolojia ya joto, lenye urefu wa kilometa 1,445 kati hizo, 1,115 zinapita Tanzania.

Mradi huo utagharimu Dola za Kimarekani bilioni 3.5 na utazalishaji ajira 10,000 wakati wa ujenzi na utasafirisha mapipa bilioni 6.5 ya mafuta yaliyogundulika katika bonde la ziwa Albert nchini Uganda kwenda Bandari ya Tanga, Tanzania.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akilakiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda, Mhe. Sam Kutesa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebbe alipowasili nchini Uganda kwa ziara ya kikazi ya siku moja jana. **PICHA: IKULU**

# Mbowe asimulia akaunti zake zilivyofilisiwa

**Na Eneck Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesimulia namna ambavyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilivyofilisi akaunti zake, biashara kiasi cha kukimbilia nje ya nchi kuwekeza.

Aidha, CHADEMA imemwandikia Rais Samia Suluhu Hassan, barua ya kuomba kuzungumza naye.

Akielezea jinsi TRA zilivyomuumiza, alisema Novemba 23, 2018, yeye na aliyekuwa kiongozi mwezake (Mbunge wa Tarime Mjini), Ester Matiko, ambao waliondolewa dhamana katika kesi ya uchaguzi walipelekwa gerezani walikokaa kwa miezi minne, na mwisho wa mwenzi ule TRA iliandika barua kudai kuwa kampuni yake moja inadaiwa Sh. bilioni mbili, jambo ambalo siyo kweli.

"Unapoidai kampuni Sh. bilioni mbili maana yake imetengeneza faida kwa mwaka ya bilioni 12 na mauzo yake ni bilioni 50, hii ni kampuni yangu yenye hoteli kifamilia ndogo ambayo huwezi kutegemea iwe na kipato kama hicho kwa miaka 20, waliniandikia TRA wananipa siku 30 nilipe au nilipeleke pingamizi ya kile ambacho wamekiona ni kodi halali," alisema jana na kuongeza:

"Yote haya yalifanyika wakijua vizuri sana nipo gerezani, na gerezani huwezi kupokea barua wala barua pepe, hawakutuma barua ofisini bali kwa barua pepe yangu binafsi wakijua haitanifikia, baada ya siku 60 wakaandika barua nyingine kwamba tulikuandikia barua, lakini hukupinga mapendekezo yetu kwa hiyo tunakupa siku nyingine 30 usipojibu tutahesabu kodi hii ni rasmi na halali."

Alisema: "Nikiwa bado gerezai barua ya pili sikuipata, nanyimwa dhamana mahakamani kwanini nanyimwa dhamana sijui, nikashtuka siku 90 zimeisha hatujapewa dhamana, wakaandika barua nyingine kwa sababu hujajibu barua zetu mbili kodi yake inaongezeka na riba inafika bilioni 2.6."

"Nilivyotoka gerezani nakutana na bili, nikawaambia hii kampuni haiwezi kufika kiasi hiki, kwa miaka miwili kampuni iko Machame mlimani Kilimanjaro ya watalii wanaopanda mlimani, nilizungumza na mamlaka zote ikiwamo Rais wakadai watashughulikia."

"Hakuna kilichofanyika wakaendelea kutizama, wakafunga akaunti zote, wakachukua fedha zote, wakafunga akaunti zangu zote za kampuni na binafsi hadi niliyokuwa napokelea mshahara wa Bunge, vitu hivi sikuvisema kwa sababu yanafanyika mengi kwa Watanzania wengi, kuanzia Desemba 2018 akaunti zangu zimefungiwa."

Alisema juzi katika mazingira ya kushangaza pengine baada ya kauli ya Rais Samia, TRA walimwandikia barua kuwa kaunti wanazifungua na zuio la akaunti zako wanalifungua.

"Hivi tu tumeamua tunaondoka zuio la akaunti zako tunafungua, hamniambii fedha mlizochukua, udhalilishaji mlionisababishia, uhuni mnionifanyia, ni wafanyabiashara wangapi, na ndiyo sababu iliyonifanya niliondoke nchini, sikwenda nchi za nje za nje kama mkimbizi wa kisiasa bali nilikwenda kutafuta uwekezaji katika mataifa mengine,"alisema.

"Kila biashara niliyojaribu kufanya ilizuiwa, ilifungiwa, iliumizwa, ilibomolewa, niliona naweza kufanya biashara Dubai na Afrika Kusini kama binadamu wengine wanaoweza kuja nchini kufanya biashara kimataifa, nilikuwa nje ya nchi kutafuta uwezo wa kufanya biashara kwa sababu ndani ya nchi yangu waliapa sitafanya biashara, kosa langu ni nini ni kwa sababu mimi ni kiongozi wa CHADEMA."

"Sawa mtanifungia Tanzania hamtanifungia Afrika Kusini, Dubai na Marekani, ni lazima tukubali uhuru wa wafanyabiashara, watumishi na Watanzania kuwa kwenye jamii ya kimataifa lilinyimwa...mimi ni Mbowe ambaye ni Mwenyekiti wa chama, ni Watanzania wangapi wenye uwekezaji hapa wamekimbia taifa, ni wangapi wa mataifa mengi wamekimbia na kuhamisha mitaji, hakika ni wengi kuliko ambavyo Watanzania wa kawaida wanaelewa," alisisitiza Mbowe.

**WAOMBA KUZUNGUMZA NA RAIS SAMIA**

Alisema maneno ya rais yalikuwa mazito na kwa niaba ya CHADEMA walimwandikia barua, pamoja na mambo mengine mengi ni juu ya maneno yake yamegusa mioyo ya wengi wenye hofu ya Mungu ikiwamo CHADEMA.

"Tumeomba rasmi kukutana naye tuweze kumweleze ni kwa vipi mioyo yetu inavuja damu, na ni kwa vipi macho yetu yanatiririka machozi. Hatukusudii kumzingua nasi hatutegemei kuzinguliwa, hatuko kwenye biashara ya siasa bali tunautafuta ufumbuzi utakaotutoa kwenye mkwamo huu na utakaorejesha furaha, haki na ustawi kwa watu wetu wote."

"Tunategemea kumweleza na kumkabidhi mapendekzo kadhaa ya kuuanza ukurasa mpya katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika azima ya kujenga utengamano wa taifa letu. Kama viongozi na wanasiasa wazoefu tunatambua Rais ana majukumu mazito na kuipanga serikali yake kipindi hiki, tunaamini atatambua nafasi ya vyama vya upinzani katika kuujenga mustakabali mwema na mpya wa nchi yetu."

**KUTOSHIRIKI UCHAGUZI WOWOTE**

Alisema msimamo wa chama hicho ni kutoshiriki uchaguzi wowote hadi mwafaka wa kitaifa upatikane kuhusiana na uchaguzi na nafasi ya demokrasia.

## HABARI KITAIFA

# Lissu aomba kuzungumza na Rais Samia

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), na aliyekuwa mgombea wa Urais kupitia chama hicho mwaka 2020, Tundu Lissu, amedokeza ombi lake la kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya mashauriano ya mambo kadhaa yanayohusu hali ya kisiasa kwa sasa.

Akizungumza jana katika mkutano wa mtandaoni na wadau mbalimbali wa siasa (zoom meeting) mwanasiasa huyo, ambaye alirejea nchini Ubelgiji baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa 2020, alisema ameshaandika ujumbe wa ombi lake hilo kupitia kwa wasaidizi wa Rais Samia wiki mbili zilizopita na sasa anasubiri kujibiwa.

"Alipoapishwa Rais Samia kwa sababu nilifanya naye kazi miaka ile akiwa Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia masuala ya Muungano na alikuja kuniangalia hospitali Nairobi kama mtakumbuka, nikapeleka (kupiga) simu kwa msaidizi wake na kumwambia naomba Mama akipata nafasi uniambie nizungumze naye, bado nasubiri," alibainisha Lissu.

Kwa mujibu wa Lissu, ili nchi iendelee, ni muhimu kukawa na uhuru wa kumshauri Rais na kumwambia ukweli pale anapokosea ili arekebishe na kumwambia anayofanya vizuri ili aongeze juhudi ya kuyafanya kuliko kujiamulia mwenyewe na hatimaye kuishia kubebeshwa lawama kila wakati.

Alisema pamoja na kwamba Rais Samia alikuwa sehemu ya serikali iliyopita kwa kuwa Makamu wa Rais katika kipindi cha Hayati Dk.John Magufuli, lakini anayo nafasi ya kufanya mabadiliko pale anapoona hapakuwa sawa kwa mustakabali wa wananchi wote badala ya kuzingatia maslahi binafsi ya viongozi wachache.

"Watu wanasema huyu Mama si alikuwa sehemu ya serikali hiyo anaweza kweli? Angola wana rais mpya mwaka wa pili sasa Eduardo do Santos alikuwa Rais wa Angola kwa miaka 40 akamuachia Waziri wake wa ulinzi na akahakikisha kwamba Waziri wa Ulinzi hawezi kumgeuka wote ni watu wa MPLA," alisema Lissu.

"Hivi tunavyozungumza binti wa Rais ambaye ndiye tajiri mkubwa Angola na vile vile ana mali nyingi kuliko Wareno wengi Ureno na ana mali nyingi kuliko Wa-Brazil wengi Brazil mali zake zote zimekamatwa na anachunguzwa na serikali ya aliyekuwa Waziri wa Ulinzi kwa Rais Eduardo do Santos," alisema Lissu.

Kwa mujibu wa Lissu, Katiba iliyopo Makamu wa Rais hufanya kazi anazopangiwa na Rais na pia Rais halazimiki kuchukua ushauri wa mtu yeyote, hivyo kumtetea Rais Samia kuwa hakuwa na mamlaka ya kufanya chochote hivyo sasa ni wakati wake akiwa kama Rais ana mamlaka yote ya kusafisha yaliyotokea huko nyuma.

Aidha, Lissu alikumbushia umuhimu wa kutengeneza katiba mpya ili kuwa na mfumo wa kitaasisi ambao viongozi watawajibika badala ya kudanganywa na kile kinachoitwa nia njema za viongozi ambazo baadae huja kudhihirika kuwa ni ulaghai.

# Kaya 22 kufanyiwa utafiti wa dhahabu

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KAYA 22 za kijiji cha Nyakafulu wilayani Mbogwe mkoani Geita, zimekubali kuruhusu mashamba yao kufanyiwa utafiti kubaini kama eneo hilo lina madini ya dhabau.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Ushauri wa masuala ya kijamii wa kampuni ya utafiti ya Mabangu, Bahati Matala, alisema mashamba ya wananchi hao yameishafanyiwa utafiti.

Alisema hatua hiyo ilifanyika kwa makubaliano kati ya kampuni hiyo na kaya hizo, na kwamba mashamba yataendelea kubakia ya wananchi hao.

Wakizungumzia suala hilo baadhi ya wananchi kutoka familia hizo, walisema wanachokijua walipewa fidia Ili kuruhusu mashamba yao kufanyiwa utafiti ili kubaini kama eneo hilo kuna madini ya dhahabu.

Mmoja wa wananchi hao, Aisha Sharifu, alisema hawajauza mashamba yao kwa mwekezaji yeyote.

Naye Jason Mkilinya, alisema mashamba yao yamefanyiwa utafiti na kampeni hiyo kwa makubaliano ya fedha kidogo, lakini hawakuwa na makubaliano ya kuyauza.

Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, mkoani Geita, Martha Mkupasi, alisema kulikuwa na taarifa za upotoshaji kwamba wananchi hao wameuza mashamba yao.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.38/2021**

Ombi la **ZUBEDA MOHAMED HIGILO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **RAMADHANI ATHUMAN MGONELA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 13/04//2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 19/03/2021**

**Tanzania Portland Cement Co.Ltd**

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

**UNAOMBWA KUWASILISHA NAMBA YA UTAMBULISHO WA KULIPA KODI**

Ndugu Mwanahisa wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company (Twiga Cement),

Tunaomba utume **TIN (TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER**) yako, ili Twiga Cement waweze kutumia wakati wanafanya malipo ya Withholding Tax (kodi) inayokatwa kwenye malipo ya gawio lako. Tunaomba utume kabla ya tarehe 30.04.2021

Tunaomba uandike namba yako ya uanachama **(CDS NO)** pamoja na majina yako kama yalivyoandikwa kwenye cheti chako cha umiliki wa hisa za Twiga Cement na utume kwenye **info@cadsecurities.com** au kwenye namba **0779303030**

HEIDELBERGCEMENT

TWIGA
Minerals Corporation Limited
a partnership between Barrick Gold Corporation and the Government of Tanzania

BARRICK
NORTH MARA

**PUBLIC NOTICE**

"Barrick Gold Corporation makes its job opportunities available on the following link: https:**//www.barrick.com/English/careers/default.aspx.** No other portal or link is used by the Barrick Gold Corporation to advertise vacancies that may become available from time to time. Any employment opportunities advertised elsewhere are not affiliated with the Barrick Gold and will not be considered by the Barrick Gold Corporation for employment."

# CAG: Mikopo HESLB inaumiza watumishi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kuwapo kwa mikopo Iliyopindukia kwa watumishi bila kudhibitiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Vilevile, CAG Charles Kichere, amebaini makato makubwa yanayofanyika katika mishahara ya watumishi wanaorejesha fedha za mkopo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) yanawaumiza watumishi husika.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20, CAG Kichere anasema kwa mujibu kifungu cha tatu cha Sheria ya Maofisa Waliobainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) Sheria Na. 7 ya Mwaka 1970 kama ilivyosisitizwa na Mwongozo wenye Kumb. Na. 26/46/01/1/66 wa Novemba 28, 2012, watumishi wanatakiwa kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.

"Kama ilivyooneshwa katika ripoti zangu za miaka iliyopita, bado kuna watumishi wa umma ambao mishahara yao ya kila mwezi inapunguzwa zaidi ya 2/3.

"Uchambuzi uliofanywa katika mamlaka 35 za Serikali za Mitaa, ulibaini watumishi 3,038 waliokuwa wakipokea chini ya 1/3 ya mishahara yao. Utaratibu huu wa kukopa usipodhibitiwa unaweza kuathiri utendaji wa watumishi na kuathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Nilibaini kuwa hali hii ilichangiwa na ulipaji wa deni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambalo hutoza asilimia 15 ya mshahara wa mtumishi ambaye ni mnufaika wa mkopo," CAG anabainisha.

CAG anasema kuwa katika hali isiyo ya kawaida, alibaini watumishi wanane katika mamlaka sita za Serikali za Mitaa ambao kila mwisho wa mwezi hawapati kiasi chochote cha mshahara.

Watumishi hao wanatoka katika Halmashauri ya Jiji la Arusha (1) na Halmashauri za Wilaya za Kiteto (1), Njombe (1), Temeke (1), Rombo (3) na Same (1).

"Ninapata wasiwasi na ustawi wa watumishi hawa katika kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi.

"Hali hii inasababisha watumishi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi ili kujipatia kipato cha ziada, hali inayoweza kudumaza utoaji wa huduma kwa jamii.

"Maofisa masuuli wanapaswa kutoidhinisha mikopo ya watumishi inayozidi kiasi kilichoidhinishwa. Vilevile, ninaishauri serikali kuangalia tena kiasi cha makato ya mkopo wa elimu ya juu ili kupunguza makali kwa watumishi," CAG anashauri.



Mbunge wa Njombe, Deo Mwanyika, akichangia bungeni Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa miaka mitano mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RIPOTI YA CAG

# Zitto aibuka na hoja za Tril. 3.6/-

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, imeendelea kuwa gumzo, huku Chama cha ACT-Wazalendo kikiibuka na hoja za ukaguzi zenye jumla ya Sh. trilioni 3.6 na Dola za Marekani milioni 596.

Katika uchambuzi wa ripoti hiyo uliowasilishwa jana mkoani Dar es Salaam na Kiongozi wa Chama hicho, Zitto Kabwe, hoja hizo za ukaguzi hazihusishi za madai ya kodi zenye thamani ya Sh. trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.

Zitto alisema kuwa hoja hizo za ukaguzi ni uwiano wa asilimia 16 ya bajeti nzima iliyotekelezwa na serikali katika mwaka wa fedha wa 2019/20, ambao ndiyo umefanyiwa ukaguzi na CAG.

"Tunatarajia kuwa mamlaka husika zitachukua hatua mahususi za kujibu hoja zote kwa mujibu wa sheria kupitia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na hatimaye kusafisha hesabu za serikali.

"Hoja nyingi za ukaguzi zinajirudiarudia mwaka hadi mwaka, hivyo ni muhimu pia kwa Bunge kuhakikisha kuwa Katiba na sheria zinaheshimiwa ili kuondoa hoja sugu," Zitto alishauri.

HOJA 10 ZA ACT

Katika uwasilishaji wa uchambuzi huo wa Ripoti ya CAG, Zitto alisema chama kilijikita kwenye mambo makubwa 10 ambayo wanaona ni muhimu Watanzania kuyatambua na kuyatolea mapendekezo ili yachukuliwe hatua.

Alizitaja hoja hizo kuwa ni pamoja na makusanyo ya kodi kuwa chini, akibainisha kuwa CAG amebaini uwezo wa serikali kukusanya mapato kulinganisha na Pato la Taifa bado uko chini.

Zitto alisema nyingine ni madai ya wazabuni dhidi ya serikali kufikia Sh. trilioni 3.1, akisema CAG amebaini kwamba, mwaka 2019/20 madai dhidi ya serikali (accumulated libalities OR Payables) yalikuwa ya Sh. trilioni 3.1 kutoka Sh. trilioni 2.7 mwaka 2018/19.

"Hiki ni kiwango kikubwa sana cha fedha za watu ambazo serikali inazishikilia mkononi baada ya kupokea huduma za watu hao. Hali hii inasababisha mdororo wa uchumi kwani serikali inashikilia fedha za makandarasi, wafanyabiashara na watoa huduma na hivyo kudumaza shughuli za uzalishaji mali na wakati mwingine kufukarisha wananchi," alitahadharisha.

Hoja ya tatu ni Sh. trilioni 2.2 kutokupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, Zitto akirejea Ripoti ya CAG inayobainisha kuwa mwaka 2019/20 jumla ya Sh. trilioni 2.16 hazikuhesabiwa Mfuko Mkuu.

Zitto aliitaja hoja ya nne fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kutokana na malipo ya fedha za watuhumiwa walioamua kukiri makosa na kulipa fidia, akitaka zipelekwe Hazina na kuwarejeshea wale ambao watathibitika kuonewa katika malipo hayo.

Alirejea ripoti ya CAG akibainisha kuwa hadi kufikia Juni 30, mwaka jana. CAG alikuta kuna fedha kiasi cha Sh. bilioni 51.521 kutokana na kesi zilizomalizika katika mahakama mbalimbali kwa kipindi cha miaka sita.

"Kwa mujibu wa CAG, fedha hizi hazikutumika kwa sababu ya kukosekana kwa sheria na kanuni za matumizi yake. Tunapendekeza Rais aunde tume ya majaji, ili kupitia malalamiko ya watu wote ambao walilipishwa fedha kwa mtindo wa kukiri makosa na kulipa fedha serikalini. Wote watakaobainika kuwa walionewa, warejeshewe fedha zao na rekodi zao za jinai kufutwa kisheria," alisema.

Hoja ya tano ni ubadhirifu wa mbailioni ya shilingi uliobainika katika Mamlaka ya Bandari (TPA), chama hicho kikitaka ufanyike uchunguzi zaidi kubaini wahusika wote wa ulaji wa Sh. bilioni 3.27 zilizoibiwa kutoka akaunti za benki.

NDEGE, SGR, STIEGLER'S GORGE

Katika hoja yake ya sita, chama hicho kinashauri kufanyike ukaguzi dhidi ya uwianо wa ununuzi wa ndege za serikali na kubadili muundo wa uendeshaji wa Shirika la Ndege (ATCL), ili kupunguza hasara, kikirejesha Sh. trilioni 1.028 zilizotumika kununua ndege ili kulifufua shirika hilo.

Zitto alisema hoja yao ya saba ni CAG kufanya ukaguzi maalum wa ununuzi wa miradi ya Reli ya Kisasa (SGR) na wa kuzalisha umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere, maarufu Stigler's Gorge, ili kutambua uzingatiaji wa thamani ya fedha (value for money) na namna ya kuimalizia kwa ufanisi zaidi.

Hoja ya nane ni kutozingatiwa kwa sheria katika utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa Mwalimu Julius Nyerere wenye thamani ya Sh. trilioni sita.

Zitto alisema mradi huo unatekelezwa na Shirika la Umeme (TANESCO) kwa kupitia kitengo cha (TECU) ambaye ni mhandisi mshauri anayesimamia mradi.

"TECU ni TANROADS, TANESCO waliingia makubaliano ya hiari na TECU bila kuingia mkataba. Hatukuelezwa hili kwa sababu serikali iliamua kuendesha kila kitu gizani. Pia, hakuna mtu aliyewajibishwa TANESCO wala TANROADS, Ni kana kwamba Tanzania ilikuwa na kundi linaloweza kuvunja sheria bila kuguswa na linaloguswa bila hata ya kuvunja sheria," Zitto alisema.

Hoja ya tisa ni hasara iliyojitokeza katika Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kwa serikali kulitelekeza bomba la gesi la Mtwara, Zitto akirejea Ripoti ya CAG inayobainisha shirika kuwa na mtaji hasi wa Sh. bilioni 332 ambao umesababishwa na mkopo ambao serikali ilichukua kutoka China kwa ajili ya ujenzi wa bomba hilo.

Zitto alisema hoja yao ya 10 ni Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kushindwa kusambaza dawa, akirejea Ripoti ya CAG inayobainisha kuwa bohari hiyo inaidai serikali jumla ya Sh. bilioni 257.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20, MSD haikupewa fedha kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa 99.45," Zitto alinukuu Ripoti ya CAG.

Zitto alitoa ushauri kwa serikali akimshauri Rais Samia Suluhu Hassan kujitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kujenga mifumo madhubuti ya uwajibikaji na kuimarisha taasisi za uwajibikaji.

"Bila taasisi imara, nchi yetu haitaweza kupiga hatua kubwa za maendeleo. Miradi mikubwa kama mradi wa umeme wa Bwala la Mwalimu Julius Nyerere, mradi wa reli ya kisasa na mradi wa kufufua ATCL inaweza kugeuka kuwa miradi yenye hasara kubwa kwa taifa iwapo hatua mahususi hazitachukuliwa kuingiza utaalamu, weledi na maarifa katika utekelezaji wake," alihitimisha.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, akiongea na baadhi ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini eneo la Haydom, alipopita kukagua barabara ya Mbulu hadi Haydom Kilometa 81 inayoombewa fedha na mbunge wa jimbo hilo ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. **PICHA:**

# Serikali yatoa bei elekezi bidhaa mwezi Ramadhani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imetangaza bei elekezi kwa ajili ya bidhaa za vyakula vinavyotumiwa wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaoanza siku chache zijazo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Unguja jana, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema lengo la uamuzi huo ni kuwawezesha wananchi, hasa wale wa kipato cha chini, kutimiza ibada hiyo ya kufunga kwa wepesi na gharama nafuu.

Kwa mujibu wa maelekezo hayo ya SMZ, bei elekezi ya mchele wa mapembe itatakiwa isizidi Sh. 1,600 kwa kilo, sukari isizidi Sh. 2,000 kwa kilo na unga wa ngano nao umepangwa usizidi Sh. 1,600 kwa kilo.

"Bei hizi zitabaki hivyo kwenye masoko mpaka hapo zitakapofanyiwa mapitio na kutangazwa vinginevyo na serikali kama inavyoelezwa kwa mujibu wa sheria. Tunatoa wito kwa wafanyabiashara na wananchi wote wazingatie bei elekezi ambayo serikali imetangaza.

"Mimi binafsi nitazungukia katika maeneo mbalimbali ya biashara kujiridhisha kama kweli wafanyabiashara wanafuata maelekezo haya ya serikali na ijulikane kwamba ziko adhabu kali kwa wale watakaokiuka bei hizi elekezi," alisema waziri huyo.

Shaaban ambaye ni mmoja wa mawaziri wawili kutoka Chama cha ACT-Wazalendo walio katika Baraza la Mawaziri la Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), alisema ametangaza bei hizo elekezi kutokana na mamlaka aliyopewa kisheria chini ya kifungu cha 61 (1) cha Sheria ya Ushindani Halali na Kumlinda Mlaji Na. 5 ya Mwaka 2018.

Waziri huyo ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema bei hizo elekezi zimepatikana baada ya mchakato uliohusisha serikali na wafanyabiashara, waagizaji na wauzaji wa vyakula visiwani humo pamoja na ukaguzi wa hali ya chakula visiwani humo uliyoonyesha kuna akiba ya kutosha ya chakula.

Alisema wizara yake imeunda kikosi kazi kinachoshirikisha Tume ya Ushindani Halali ya Biashara, Idara ya Biashara na Masoko na Halmashauri za Wilaya kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo na kuchukua hatua stahiki kwa watakaokwenda kinyume cha bei elekezi.

"Kumekuwa na ada ya muda mrefu ya baadhi ya wafanyabiashara wasio na huruma wenye tamaa kutumia fursa ya mwezi mtukufu kupandisha bei kiholela hasa kwa bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, sukari na unga wa ngano.

"Tabia kama hizi za kutaka kuchuma faida kupitia mgongo wa wanaofunga hazikubaliki na mara nyingi husababisha wananchi walio wengi ambao hali zao ni duni kutekeleza ibada yao ya funga katika mazingira magumu," alisema.

Waziri huyo alitumia nafasi hiyo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kuwatakia Waislamu wote nchini mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

# Hapi aagiza msako sokoni

**Na Francis Gowin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi ,ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya msako katika maeneo ya biashara ambako wananchi wanatapeliwa bidhaa na wanaouza vifaa vya ujenzi bei kubwa.

Hapi alitoa agizo hilo juzi baada ya kufanya ziara katika masoko mbalimbali ya Manispaa ya Iringa na kubaini udanganyifu mkubwa unaofanywa na wafanyabiashara wa viazi, nyanya na vitunguu kwa kuuza bidhaa hizo kijanja kwa kupanga bidhaa hizo juu huku chini debe likiwa na uwazi mkubwa .

Alisema kuwa hawezi kufumbia macho wizi huo maana unachafua sifa ya mkoa, hivyo lazima wafanyabiashara hao wasakwe na wachukuliwe hatua kali.

"Nimeelezwa hapa kuwa kuna mtoto alipigwa na mzazi wake, baada ya kutumwa viazi bede moja ila akabambikwa lita 10 badala ya lita 20, " alisema.

Hivyo aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama vikiongozwa na Jeshi la Polisi kufanya msako mkali hasa kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema tabia hiyo ya wizi imeendelea kuota mizizi katika masoko na nje ya masoko ya Mkoa wa Iringa, jambo ambalo linaumiza wananchi na kuchafua sifa ya Mkoa.

Awali wafanyabiashara wa soko la mashine tatu walimthibitishia mkuu wa mkoa kuwapo kwa udanganyifu huo kwa mazao kama viazi, nyanya na vitunguu wakati wale wa mchele, mahindi wamekuwa wakiongeza ukubwa wa ndoo kwa mchanga wa moto kuweka kwenye ndoo zinazotumika kununulia mazao kwa wakulima.

# Mjadala bajeti ijayo kuanza wiki hii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAJETI ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha itaanza kujadiliwa kesho bungeni, wizara mbalimbali zitakapowasilisha makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka huo.

Leo, wabunge wanahitimisha mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26.

Bajeti Kuu ya Serikali inatarajiwa kusomwa Juni 17, mwaka huu baada ya kupitishwa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara zote 23.

Kwa mujibu wa ratiba ya Mkutano wa Tatu wa Bunge, baada ya kuhitimishwa majadiliano hayo, kesho zitaanza wizara zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo makadirio yake yatajadiliwa kwa siku nne.

Baada ya ofisi hiyo, itafuata Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ambazo zitajadiliwa kwa siku tano.

Baada ya mapumziko ya Sikukuu ya Muungano Aprili 27, mwaka huu, yatasomwa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, yakifuatwa na ya Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Madini ambazo makadirio yake yatajadiliwa kwa siku moja kila moja.

Aprili 30, mwaka huu, itakuwa zamu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kujadiliwa kwa siku mbili ikifuatwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Wizara zingine ambazo mijadala yake itafanyika kwa siku mbili kila moja ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati.

Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Fedha na Mipango yatasomwa na kujadiliwa kwa siku moja kila moja.


**SALAAM PRE&PRIMARY SCHOOL**

**(P O BOX 104418:0658808862** Chamazi Temeke Dsm)

The administration of Salaam Pre and Primary School wishes to inform the public that we are in need of teachers:

The applying persons should have the following qualities:

a) Should be able to express themselves fluently in English.
b) Should be qualified with minimum qualification is a degree in Education.
c) Should be able to teach science subjects, mathematics and English.
d) Should be able to work with minimal supervision.
e) Should be able to turn for work if called upon to do so outside the usual working hours like late in the evening, over the weekends or to conduct lessons very early before seven thirty in the morning.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maandalizi Simba robo fainali CAF yaanze sasa

**WAWAKILISHI** wa Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wametinga robo fainali ya michuano hiyo kwa kishindo baada ya kuibuka kinara wa Kundi A, lakini pia wakiwa miongoni mwa timu tatu zilizofanya vizuri zaidi kutoka katika makundi yote manne.

Simba ambayo ilikuwa Kundi A ambalo linatajwa kuwa gumu zaidi likiundwa na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan, imemaliza hatua hiyo ikiwa kileleni na ponti 13 sawa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kutoka Kundi B na Wydad Casablanca ya Morocco kutoka Kundi C.

Lakini pia ubora wa hali ya juu ulioonyeshwa na wachezaji wa Simba, wameifanya klabu hiyo kuwa moja ya timu tishio zaidi msimu huu na kupewa nafasi ya kufika fainali katika michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Kwa sasa hakuna nafasi tena kwa Simba kukutana na Al Ahly hatua ya robo fainali ama nusu fainali, hivyo kinachosubiriwa ni kuona endapo itapangwa na timu ipi kati ya zilizomaliza nafasi ya pili kutoka Kundi, B, C na D ambazo ni CR Belouizdad na MC Alger za Algeria, ama Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Nipashe tunatambua hatua inayofuata ndiyo ngumu zaidi kuliko ya makundi, kwa kuwa timu zote zilizotinga robo fainali ni bora na haina maana kwamba zilizomaliza nafasi ya pili ni dhaifu.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba katika hatua hii ni mechi za mtoano nyumbani na ugenini, hivyo timu itakayopata matokeo mazuri ya jumla ndiyo itakayotinga nusu fainali ambako huko nako mtaendelea kutumika mfumo huo wa mtoano kabla ya fainali ambayo itapigwa mechi moja katika uwanja usiohusiana na timu yoyote (neutral graound).

Kwa mantiki hiyo, wakati huu Simba ikisubiri Aprili 30, mwaka huu siku ambayo itachezeshwa droo ya hatua ya robo fainali kujua mpinzani wake, inapaswa kuanza mapema maandalizi ya nguvu hususan kuinoa vema safu yake ya ushambuliaji.

Hatua ya robo fainali na hata nusu fainali, Simba inapaswa kuwa makini zaidi kwa kutumia kila nafasi na ikiwezekana kupata ushindi wa mabao mengi kwenye mechi ya awali ili kujiweka katika mazingiza mazuri ya kusonga mbele katika mechi ya marudiano.

Kinachoweza kuihakikishia timu yoyote kusonga mbele ni idadi kubwa ya mabao, hivyo kwa timu kama ya Simba ambayo imekuwa ikitengeneza nafasi nyingi na ikiishia kubadili chache kuwa mabao, kuna haja ya benchi la ufundi la timu hiyo likiongozwa na Kocha Mkuu Mfaransa Didier Gomes, kuanza kulifanyia kazi suala hilo mapema.

Katika hilo, tunafahamu Gomes atakuwa na uwanja mpana wa kulifanyia kazi kwa kuwa kikosi chake kinarejea kuendelea na mechi za Ligi Kuu Bara pamoja na Kombe la FA, hivyo tunamkubusha kumulika zaidi safu yake ya ushambuliaji katika mazoezi ya kila siku na hata kupitia michezo ya ligi watakayocheza.

Tukiwa wadau wakubwa na namba moja wa michezo nchini, tunatamani kuona Simba ikifika mbali zaidi kwenye michuano hiyo na kilele chake msimu huu kiwe kulitwaa taji hilo kubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika, kwa kuwa kwa kufanya hivyo kuna faida kubwa sana kwa soka la Tanzania.

Tunafahamu kadri Simba inavyofanya vizuri katika michuano hiyo, inaongeza pointi kwa Tanzania kuwa nafasi kubwa ya kuingiza timu nne kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF); mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Si hilo tu, bali pia kufanya vizuri kwa Simba kutazidi kuwafanya mawakala wengi wa kusaka vipaji kulimulika soka la Tanzania hivyo kuongeza ajira kwa wachezaji wa soka nchini, lakini pia kutawavutia wadhamini wengi kuja kuwekeza kwa klabu za hapa nchini, hivyo ni wakati sasa kwa wawakilishi hao wa nchi kuanza kujipanga vema kuelekea hatua inayofuata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### TFF ifanyie kazi malalamiko ya Biashara Uwanja wa Karume

Na Adam Fungamwango

**MARA** baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Biashara United dhidi ya Polisi Tanzania kulitokea vurugu kubwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

Picha za video zilizoonyeshwa na vyombo mbalimbali vya habari vinaonyesha jinsi askari polisi waliokuwa wakidhibiti baadhi ya mashabiki. Lakini pia baadhi ya mashabiki walionekana hawakubali na kutaka kupambana na askari polisi, ambapo nao ikabidi watumie nguvu za ziada.

Haijajulikana mara moja sababu ya vurugu hizo ni nini, lakini ndani ya uwanja timu hizo zilitoka sare bao 1-1, matokeo ambayo yasingeweza kusababisha hasira na mtafaruku wote huo.

Hata hivyo, dalili za viashiria vya vurugu vilianza kuonekana mapema baada ya Biashara United kudai kuwa Jeshi la Polisi mjini Musoma lilipeleka askari watano kwenye Uwanja wa Karume mjini humo kwenda kulinda uwanja kwa ajili ya mechi hiyo iliyochezwa saa nane mchana.

Inadaiwa askari hao wakiwa na sare walipokuta geti limefungwa waliruka ukuta wa uwanja huo. Hata hivyo, Jeshi la Polisi Mara, lilikanusha kutuma askari hao.

Msimamizi wa uwanja huo ambaye ni Katibu wa Chama cha Soka mkoani Mara, Samuel Mziba, akanukuliwa akidai kuwa alishangazwa na kitendo hicho kwa sababu hakuwa na taarifa.

Mwenyekiti wa Biashara United alisema kuwa baada ya mechi kumalizika, askari polisi walianza kupiga mashabiki wa timu yake, kitu ambacho alisema si taratibu za kisoka.

"Soka ina taratibu zake. Polisi wafuate utaratibu na wasipende kutumia nguvu pasipo sababu," alisema mwenyekiti huo.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema kuwa kilichotokea ni kwamba baada ya mechi kumalizika, mashabiki wa Biashara United walianza kufanya vurugu. Taarifa zinaeleza kuwa tayari Biashara United imepeleka malalamiko yake Shirikisho la Soka nchini (TFF) kupitia Bodi ya Ligi (TPLB).

Ukilifuatilia tukio hili, ukisikiliza maneno ya viongozi hao, lakini pia ukirejea matukio ya huko nyuma unakuta kuna kitu kinatakiwa kufuatiliwa kwa ukaribu na Bodi ya Ligi. Kwanza inaonekana huenda askari Polisi wanafanya hivyo kwa kuisaidia timu yao ya Polisi Tanzania.

Miaka michache nyuma kulikuwa na tabia kama hii kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwa timu za Majeshi la Ulinzi. Timu nyingi za aina hiyo zilikuwa zinakwenda na wanajeshi ambao walikuwa wanatuhumiwa kupiga mashabiki wa timu za kiraia, lakini pia hata waamuzi wanakuwa matatani.

Baada ya TFF kulivalia njuga suala hilo, ikiwamo kuzifungia baadhi ya timu, lakini pia na kutoa elimu, hili limepungua sana. Kinachotakiwa sasa kwa TPLB na TFF ni kufanya uchunguzi kujiridhisha kama ni kweli askari polisi wa Mara walitumika kwenda kulinda uwanja, au wamekuwa na tabia ya kuisaidia timu yao ya Polisi Tanzania kwa kutumia mabavu ili jambo hili likomeshwe, kwani likiachwa kuna siku litaleta madhara.

Upande wa pili wa shilingi ni kwa muda mrefu sana Uwanja wa Karume umekuwa ukilalamikiwa na timu nyingi kwa fujo.

Tangu Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza, baadhi ya timu zimekuwa zikilalamika kuwa zinapokwenda huko zimekuwa zikikumbana na misukosuko ndani na nje ya uwanja, lakini si TFF wala Bodi ya Ligi imekuwa ikilifuatilia hilo.

Inasemekana mashabiki wa Biashara United wamekuwa wakiwasumbua hata makocha na viongozi wa timu pinzani wanapokuwa uwanjani.

Si Bodi ya Ligi wala TFF iliyotoka hadharani na kusema wamefuatilia suala hilo na kukuta ni kweli, au halina ukweli wowote.

Inawezekana askari polisi kwa kujua hilo wakaamua kufanya hivyo kwa kuilinda timu yao baada ya kuona hakuna adhabu yoyote au tamko lolote linalotolewa na mamlaka ya soka kwa mambo yanayofanyika kwenye Uwanja wa Karume.

Pia inawezekana askari polisi wa mkoa wa Mara wanajua kinachozipata timu zinazokwenda huko, hivyo wao waakaamua kuilinda timu yao ili isikumbane na kadhia ambazo timu nyingine inazipata.

Kama hili limewafikia mezani, ni wajibu sasa wa TFF na Bodi ya Ligi kufanya uchuguzi na kufuatilia malalamiko yote juu ya polisi kutumia nguvu kubwa ya nje ya uwanja kwa mashabiki pale timu yao inapocheza, lakini pia mashabiki wa Biashara United na Uwanja wa Karume ambao unasemekana si salama kwa timu za Ligi Kuu zinapokwenda kucheza.

# RC apiga marufuku watoto wa kike kuchunga mifugo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amepiga marufuku watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo, ili kuwaepusha na vishawishi vya kufanya ngono na kupata mimba za utotoni, hatua ambayo itawasababishia kukatisha masomo yao.

Telack alitangaza marufuku hiyo juzi kwenye kikao cha majadiliano cha kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, kilicho andaliwa na Shirika la Msichana Initiative ambalo linatetea haki za watoto.

Alisema moja ya changamoto zinazochochea mimba za utotoni mkoani humo, ni watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo maporini, hatua ambayo inawapa mwanya wa kukutana na wanaume na kisha kujamiiana na kuambulia ujauzito.

"Nawasihi wazazi na walezi mkoani Shinyanga, achaneni kabisa na tabia ya kupeleka watoto wa kike kwenda kuchunga mifugo, bali kazi hiyo ifanywe na wanaume ili kuwalinda dhidi ya mimba za utotoni na kutozima ndoto zao," alisema Telack.

Aidha, alisema kwa takwimu za utafiti zilizofanywa na Shirika la maendeleo ya watu na afya (TDHS) 2010, Mkoa wa Shinyanga ulitajwa kuongoza kwa mimba na ndoa za utotoni asilimia kwa 59, lakini kwa sasa wameshapiga hatua kubwa kuzipunguza, huku wakiendelea na mikakati ya kuhakikisha matukio hayo yanabaki kuwa historia.

Naye Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenani, akizungumza kwenye kikao hicho, alisema kuna haja kwa wadau na Serikali kuunganisha nguvu ya pamoja kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, ikiwamo kuifanyia marekebisho ya haraka Sheria ya ndoa ya Mwaka 1971 ambayo ni kandamizi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeka Gyumi, alisema bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha tatizo hilo linakoma kabisa nchini, pamoja na kila mkoa kuweka mikakati yake namna watakavyo pambana kukomesha mimba na ndoa za utotoni, kama walivyofanya Mkoa wa Shinyanga.

# Hoja mbili nyeti zawasilishwa bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

TAASISI ya WAJIBU imewasilisha mapendekezo mawili kwa Bunge la Tanzania, ikilishauri kuyafanyia kazi ili kuongeza uwajibikaji nchini.

Mapendekezo hayo ni pamoja na Bunge kuiagiza serikali kuanzisha utaratibu wa ripoti ya Msajili wa Hazina kuwasilishwa bungeni, ili kutoa nafasi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuipitia.

Yona Killagane, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya WAJIBU, aliwasilisha mapendekezo hayo juzi kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, wakati wa mafunzo maalum kwa wajumbe wa kamati tatu za Bunge (PAC, LAAC na PIC) yaliyoendeshwa na taasisi hiyo bungeni jijini hapa.

Alisema kwa kutambua kwamba PIC ni kamati changa, taasisi yao inapendekeza Bunge limtake Msajili wa Hazina awe anaandaa ripoti za taasisi zote anazisimamia na ripoti hizo zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kisha kuwasilishwa bungeni ili zifanyiwe kazi na kamati hiyo.

Katika pendekezo la pili, Killagane alisema kuna haja ripoti ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iwe inawasilishwa bungeni ili kutoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa.

"Taarifa ya PCCB (TAKUKURU) ni kazi nzuri na nyeti. Tunapendekeza iwafikie pia wananchi ili washiriki mapambano dhidi ya rushwa. Ripoti ya PCCB iliyowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 28, mwaka huu, iwasilishwe bungeni ili iwe wazi na ijadiliwe kuwapa fursa wananchi," Killagane alipendekeza.

Mwenyekiti huyo pia alimpongeza Spika Ndugai kwa kuliongoza Bunge kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu, akidokeza namna chombo hicho kilivyosimama imara hata baada ya kufariki dunia kwa Rais John Magufuli.

Killagane pia alimshukuru Spika Ndugai kwa kuipa ushirikiano taasisi hiyo inayoongozwa na CAG wa zamani, Ludovick Utouh, na kuialika bungeni kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati hizo tatu.

**SPIKA NDUGAI**

Akifungua mafunzo hayo, Spika Ndugai alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wajumbe wa kamati hizo nyeti kwa kuwa yanawajenga uwezo kufanya kazi zao kwa weledi. Spika Ndugai pia aliwakumbusha wajumbe wa kamati hizo kutunza siri na kutojihusisha na vitendo vya rushwa katika kutekeleza majukumu yao.

"Wajumbe wa kamati hizi tunategemea sana katika utendaji wa shughuli zetu bungeni. Mafunzo haya ni muhimu sana kwetu maana yanatujengea uwezo wa kufuatilia na namna ya kufanya mahojiano na maofisa wa tunaowaita kwenye kamati hizi," alisema. Spika Ndugai aliwaagiza viongozi wa kamati hizo kuwasilisha kwa Kamati ya Uongozi ya Bunge majina ya wajumbe wenye tabia ya kuvujisha siri za kamati ili wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Grace Tendega, alisema; "Tunawashukuru sana WAJIBU kwa mafunzo haya, tunakuahidi Mheshimiwa Spika, tulichokipata hapa tutakifanyia kazi kwenye utekelezaji wa majukumu yetu. "Tunakushuru Mheshimiwa Spika kwa kutenga muda wako na kushiriki na sisi kwenye mafunzo haya muhimu."



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, akizungumza kwenye kikao cha majadiliano namna ya kuendelea kupambana kutokomeza mimba na ndoa za utotoni mkoani humo, kilicho andaliwa na Shirika la Msichana Intiative ambalo linatetea haki za watoto hapa nchini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Trafiki wakatazwa kukamata bodaboda, bajaji kwa nguvu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewataka askari kuacha mara moja matumizi ya nguvu wakati wa kuwakamata madereva bodaboda na bajaji barabarani, kwa kuwa hali hiyo inahatarisha maisha yao.

Waziri Simbachawene aliyasema hayo jana wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa tawi la Polisi Tanzania.

Alisema askari wengi barabarani wamekuwa wakitumia msuli kufukuzana na madereva bodaboda au bajaji kwa kutumia nguvu badala ya sheria, jambo ambalo sio sahihi.

Simbachawene alisema kinachotakiwa ni kutumia sheria ambayo itamtia hatiani dereva kulingana na kosa alilotenda.

"Hiki kitu huwa kinanishangaza sana kwasababu sheria zipo kwanini askari utumie misuli kukimbizana na dereva bodaboda?" alihoji Simbachawene.

Alisema wito wake ni vema jeshi hilo likafanya kazi kwa juhudi, weledi na maarifa ili kuunga mkono Serikali na kuhakikisha kila eneo linakwenda sawa kiutendaji.

Hata hivyo, alivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kupiga vita mambo mbalimbali ya kihalifu ikiwamo biashara ya madawa ya kulevya, Panyaroad na vitu vingine ambavyo vilikuwa vikihatarisha usalama wa watu.

Alisema askari wanapaswa kufanya kazi kwa bidii, huku akiwasihi watarajie mambo makubwa kutoka katika serikali yao.

Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu wa jeshi hilo, Benedict Wakulyamba, ambaye ni Kaimu Mwenyekiti wa Baraza hilo akizungumza kwa niaba ya IGP, alilitaka Jeshi hilo kufanya kazi kwa bidii ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

# Wakala wa mapato h'shauri matatani

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKALA wa ukusanyaji ushuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Darasa Ally Mwamba, anashikiliwa kwa mahojiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), akidaiwa kujipatia Sh. 3,261,000 kinyume cha Sheria.

Mkuu wa taasisi hiyo, Abnery Mganga, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari na kwamba Mwamba amekamatwa baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasiri wao, kwamba mtuhumiwa amekuwa na tabia ya kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2013 hadi 2015.

"Huyu Mwamba alipangiwa kukusanya ushuru kituo cha eneo la soko katika Mji Mdogo wa Masoko," alisema Mganga.

Mganga alisema Januari 2, 2015 Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kilwa ilipokea taarifa kutoka kwa msiri, kwamba kuna upotevu wa fedha za mapato katika Halmashauri ya Wilaya hiyo, hali iliyowalazimu kufanya uchunguzi.

Mganga alisema baada ya kupata malalamiko hayo, walianza kufanya uchunguzi uliowawezesha kupata ushahidi wa kutosha, kwamba mtuhumiwa alijihusisha na vitendo vya rushwa na kujipatia Sh. 3,261,000 kwa njia ya udanganyifu.

"Tayari uchunguzi tumeukamilisha na jalada tukalipeleka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP)," alisema na kuongeza kuwa kibali kimetolewa na watamfikisha mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.

Alisema Mwamba anakabiliwa na mashtaka matano, likiwamo matumizi mabaya ya nyaraka kumdanganya mwajili, uchepushaji fedha, matumizi mabaya ya mamlaka, kughushi hesabu pamoja na kujipatia kiasi hicho cha fedha na kujipatia manufaa kinyume cha Sheria.

Alisema kutokana na kitendo hicho, Mwamba anakabiliwa na makosa hayo chini ya Sheria Namba 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 31 kanuni ya adhabu sura ya 16 mwaka 2007, na kwamba mtuhumiwa atafikishwa kortini muda wowote kuanzia sasa.

# Mwanyika atoboa siri ya kuufikia uchumi mkubwa

**Na Gwamaka Alipipi**

MBUNGE wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, amesema ili Taifa lifikie uchumi wa juu, ni lazima serikali iishirikishe sekta binafsi, pamoja na kupunguza urasimu katika uwekezaji.

Amesema pia ni lazima Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wabadilishe mitazamo yao kwamba sekta binafsi wanaweza kusaidia katika kukukuza wa uchumi wa nchi.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki bungeni jijini Dodoma, wakati akichangia Mpango wa Maendelea wa Tatu wa Miaka Mitano, uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba,

Mwanyika alisema: "Ni ukweli usiopingika kwamba ili tukitaka uchumi wetu ukue sekta binafsi haikwepeki, sekta binafsi ni muhimu, tuiwezeshe ili ikuze uchumi."

Aliongeza: "Kinachojitoleza ni kwamba imeingia katika matatizo makubwa sana na baadhi ya wawekezaji wamekwamishwa tamaa, wengine wamefunga biashara.

Hii haina afya kwa uchumi wetu na mpango wetu. Nimpongeze Rais Samia kwa kutoa kauli ambayo imetoa mwanga kwa nchi yetu."

Mwanyika alisema uhusishwaji wa sekta binafsi upo katika ngazi ya sera pamoja na masuala ya kikodi.

Alibainisha kwamba setka binafsi ina vyombo maalum vya kufanya mazungumzo na serikali, hali hiyo imekuwa ikifanyika lakini matatizo ambayo yamekuwa yakiwapata yanafahamika.

"Wote tunajua kuna blue print, lakini urasimu bado unaua sekta binafsi. Blue print ni karatasi tu, tunachohitaji ni kuwa mtazamo chanya katika ubongo wetu na viongozi wa serikali kuanzia Benki Kuu, TRA wabadilishe fikra zao kwamba sekta binafsi wanaweza kubadilisha uchumi, vinginevyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu" alisema Mwanyika.

Alisema kinachoua uchumi wa nchi ni hatua ya serikali kufanya kila kitu peke yao pasipo kuwashirikisha sekta binafsi, kwamba hata baadhi ya miradi imekuwa ikijengwa na serikali ikishirikiana na taasisi za umma.

Mwanyika alisema: "Sheria tumetunga lakini nawaambia sheria hizi zitabaki kuwa makaratasi endapo hakutakuwa na mikakati mizuri".

Kuhusu Kilimo, Mwanyika alisema bado sekta ya kilimo itabakia kuwa sekta kiongozi, lakini inakabiliwa na matatizo makubwa.

Alisema sekya ya kilimo inahitaji kichocheo kikubwa ambacho ni miundombinu wezeshi.



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi (wa pili kushoto) akikagua ukarabati wa ujenzi wa Msikiti Mkuu wa Gadafi, mkoani Dodoma jana, kushoto ni Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, kulia ni Mwenyekiti wa BAKWATA Mkoa, Jafari Mwanyemba na wa pili kulia ni Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya, Bashiru Omari. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# CRDB yatoa mil. 10/-, chakula kwa watoto uhitaji maalum

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya CRDB, imetoa sadaka ya Sh. milioni 10 pamoja na kilo 150 za chakula kwa vituo vitano vya watoto wenye uhitaji maalum, vilivyopo katika wilaya za jijini Dar es Salaam, ikiwa ni maandalizi ya mfungo wa mwezi wa ramadhani.

Vituo vilivyopokea msaada huo ni Tarbia, Irshad Islamic, Amani Foundation for Orphans, Hiyari Orphans na Busara Orphans.

Mkurugenzi wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, akikabidhi msaada huo akiambatana na familia yake pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo, alisema msaada huo utasaidia kwa ajili ya futari yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa watoto hao.

Nsekela alisema sadaka hiyo ni sehemu ya shukrani ya familia yake na mwendelezo wa benki hiyo, kutoa msaada kwa makundi maalum pamoja na kuandaa futari kwa ajili ya wateja wake hususan kipindi cha ramadhan.

"Tukikaribia kuanza mwezi mtukufu wa ramadhan, mioyo na fikra vipo katika kumnyenyekea muumba tumeona ni jambo la faraja kujumuika kwa pamoja na watoto yatima katika ibada hii ya funga kwa kuwapatia msaada wa futari," alisema Nsekela.

Hafla hiyo ilifayofanyika katika viwanja vya Karimjee na kutanguliwa na ibada ya Ijumaa, iliyoongozwa na Imam, Haroub Khamis katika Masjid ya Karimjee, mwishoni mwa wiki, Nsekela alisema kuwa msaada pia utavifikia vituo vya watoto yatima katika kanda zote nchini.

Alibainisha ilivyo muhimu kuwasaidia watu wenye mahitaji hasa kipindi cha mfungo ili waweze kutimiza funga yao kikamilifu.

"Kutoa msaada kwa watu wasiojiweza ni kujitafutia thawabu, lakini pia kunasaidia kudumisha upendo kwa ndugu, jamaa, marafiki na jamii kwa ujumla wake.

"Hata katika Quran takatifu Surah Al-Baqarah aya ya 2:83, Mwenyezi Mungu ametuamrisha kuwasaidia yatima na wasiojiweza," aliongezea Nsekela.

Kwenye msaada huo kila kituo kilipatiwa unga wa ngano kilo 50, sukari (50), maharagwe (50) pamoja na tambi pakiti 30, tende na mafuta ya kula lita 20.

Pia vilikabidhiwa njugu kilo 20, sabuni pamoja na maziwa ya unga, na majani ya chai.

Akizungumza mara baada ya kupokea msaada huo kwa niaba ya vituo vya watoto yatima, Sheikh Issa Othman Issa, alimshukuru Nsekela na familia yake pamoja na wafanyakazi wa Benki ya CRDB, kwa msaada huo.

"Mafundisho ya Mtume SAW yanatuambia atakayemfuturisha aliye na swaum atapata thawabu kama zake bila ya mwenye swaum kupungukiwa na kitu.

"Kwa niaba ya vituo hivi na watoto hawa niwashukuru sana na Mwenyezi Mungu aendelee kuibariki Benki yetu ya CRDB," alisema Sheikh Issa.

Mkurugenzi wa Kituo cha Amani Foundation for Orphans, Zubeida Abdallah, alishukuru kwa msaada huo na kwamba umekuwa faraja kwa watoto hao na utawasaidia kukamilisha funga yao.

"Mkurugenzi mtendaji kwa niaba ya vituo hivi nikushukuru sana kwa msaada huu, nichukue pia fursa hii kuwakaribisha katika vituo vyetu ili tuweze kujadiliana kwa pamoja namna bora ya kuwasaidia watoto wetu hawa," alisema Zubeida.

HABARI KITAIFA

## Samia awakosha wananchi Lindi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKAZI kadhaa wa Mkoa wa Lindi wameeleza kutiwa matumaini na hotuba zinazotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan

Wananchi hao Issa Juma, Abdallah Saidi (Manispaa ya Lindi), Mwanaisha Mussa na Yusufu Abdallah (Nachingwea), Deo Selemani na Ally Isumaili (Kilwa) kwa nyakati tafauti walisema baadhi ya mambo wanayofurahishwa nayo ni kuwataka watendaji wa Serikali, wakiwamo mawaziri wawajibike kwa wananchi, kuruhusu vyombo vya habari vilivyofungiwa vifanye kazi ya kuhabarisha jamii na kuwa na uhusiano mzuri na wafanyabiashara ili taifa liweze kupata mapato yake.

Walieleza kuwa uamuzi huu wa Rais Samia unarejesha imani kubwa ya wananchi kwa serikali yao.

Hata hivyo, walimwomba mkuu huyo wa nchi kuruhusu kufanyika kwa maonesho ya siku ya wakulima (Nanenane), kwani yamekuwa yakiwasaidia wananchi kupata elimu ya kilimo na ufugaji.

## Watoto, mvuvi wafa maji

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watatu akiwamo mvuvi na watoto wawili, wakazi wa mji mdogo na mkongwe wa Kivinje, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wamekufa maji, baada ya kuzama katika Bahari ya Hindi.

Tukio hilo lilitokea Aprili 7 na miili yao iliopolewa Ijumaa mchana, huku ikielezwa kuwa watoto hao walikuwa wakichezea maji wakati mvuvi alikuwa anavua samaki.

Mohamedi Peta, Mwenyekiti mstaafu wa Mji Mdogo wa Kivinje na Diwani wa Kata hiyo, Bakari Arobaini,

aliwataja waliokufa ni Selemani M'bwana (38) (Mvuvi),Yusufu Natepe (11) na Selemani Hamisi (12).

Mashuhuda walisema M'bwana alifariki alipokuwa baharini akivua samaki, wakati watoto hao wamekufa wakiwa wanacheza majini wakitumia mitumbwi iliyokuwa imeegeshwa maeneo ya pwani karibu na fukwe.

Mashuhuda hao walisema M'bwana aliondoka nyumbani kwao kwenda baharini kwa ajili ya kuvua samaki, hata hivyo hakurejea, hali iliyoleta taharuki kwa wananchi kuanza kuwatafuta na kufanikiwa kuipata miili yao Ijumaa mchana ikielea kwenye maji.

Natepe Yusuf na Hamisi Selemani, wazazi wa watoto hao, walithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kupokea taarifa za tukio hilo, lakini alisema atatoa taarifa leo, kutokana na kukabiliwa na majukumu mengi.

"Taarifa hiyo imenifikia ofisini kwangu lakini leo sitaweza kukuelezea kwakuwa nina ugeni ndugu yangu, "alisema Kamanda Kintikwi.

# Mamia wapewa elimu chakula chenye lishe

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAASISI ya sekta binafsi inayojishughulisha na kuendeleza sekta ya bustani Tanzania (TAHA,) imetoa elimu ya lishe kwenye vikundi vinne vya kinamama vyenye wanachama 350 ili kusaidia jamii kuondokana na tatizo la udumavu kwa watoto wadogo.

Vikundi vipo Kata za Lunguya, Shilela na Segese Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga.

Akitoa elimu hiyo jana Mratibu wa lishe na Jinsia wa taasisi hiyo, Salome Stephen, alisema lengo la utoaji wa mafunzo hayo ni kuwapatia uelewa wananchi juu ya masuala ya lishe kuhusu ulishaji bora wa watoto ili kuepukana na tatizo la udumavu kwa watoto wadogo.

Alisema kinamama wengi wanapata ujauzito, huku wakiwa hawatambui namna bora ya maandalizi ya chakula chenye lishe wakati wa ujauzito na kusababisha kujifungua watoto wenye uzito pungufu, kupungukiwa damu na kuhatarisha afya zao.

Aidha, Stephen alisema asilimia kubwa ya kinamama wanaandaa chakula ilimradi kula na kushiba na kusababisha mtoto wao kukua kimwili badala ya kukua kiakili, hali hiyo imekuwa ikisababisha mtoto kushindwa kutunza kumbukumbu hasa akiwa masomoni.

Pia aliwataka kinamama kunyonyesha watoto wao ipasavyo kipindi chote cha siku 1,000 za ukuaji wa mtoto ili kujikinga na kansa ya matiti pamoja na saratani ya shingo ya uzazi.

Nae Diwani wa Lunguya, Benedictor Manwari, alisema wamekuwa wakiwahamasisha wajawazito kuhudhuria kliniki kipindi chote cha ujauzito na kujifungulia katika vituo vya afya ili kupata elimu ya maandalizi ya chakula chenye lishe kwa watoto wao wanaokuwa wamejifungua. Pia alisema wakati wa mikutano ya hadhara, wamekuwa wakiwaalika wataalamu wa lishe kutoka wilayani na kutoa elimu ya namna ya maandalizi ya chakula chenye lishe kwa watoto lengo likiwa kuendelea kupambana na tatizo la udumavu.

Christina Stephen, Mwenyekiti wa Wanawake Vijana Umoja Kata ya Lunguya, alisema ukosefu wa elimu ya lishe unasababisha kuandaa chakula kienyeji na kuwalisha watoto makapi na kwamba elimu waliyopata itasaidia kutatua changamoto ya tatizo la udumavu.

Nae Leah Mathius, mkazi wa Kijiji cha Marito, alisema ukosefu wa kipato cha uhakika ndani ya kaya unasababisha baadhi ya familia nyingi kushindwa kula chakula bora chenye lishe, na kwamba imekuwa ikisababisha kuanza kuwapatia chakula watoto wadogo kabla ya muda wa kula.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deogratius Ndejembi, akizungumza na wananchi na wanufaika wa TASAF Kijiji cha Nkala wilayani Momba wakati wa ziara yake ya kikazi kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika kijiji hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Washauri elimu kwa watoto wenye usonji

**Na Romana Mallya**

FAMILIA na wadau wanaojihusisha moja kwa moja na watoto wenye usonji (autism), wameungana wakiomba serikali kuweka mfumo ambao utaliwezesha kundi hilo kupata elimu kuanzia chini hadi ngazi za juu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana jijini Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya kidunia ya siku ya kujengeana uelewa dhidi ya kundi hilo, walisema moja ya tatizo wazazi na walezi wanalokutana nalo ni watoto wao kushindwa kuendelea na masomo ya sekondari kama watoto wengine.

Maadhimisho hayo yameandaliwa na taasisi ya Lukiza Autism Foundation (LUKIZA), inayojihusisha na tatizo la usonji ambalo limewaleta pamoja wazazi na walezi wenye watoto wa matatizo hayo ili kupaza sauti zao kupitia kauli mbiu isemayo, "Elimu Jumuishi, Jamii Jumuishi, Kazi Jumuishi."

Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa LUKIZA, Hilda Nkabe, alisema ana mtoto wa miaka 15 ambao ni umri wa kuendelea na masomo ya sekondari lakini mpaka sasa hafahamu ampeleke wapi ili apate fursa hiyo.

Mkurugenzi wa kituo cha afya cha THT, Dk. Isaac Maro ambaye pia anaendesha kipindi cha njiapanda, Afyacheck, kupitia redio ya Clouds, alisema naye ana mtoto mwenye matatizo hayo na matatizo ni hayo hayo.

"Ilinichukua miezi sita kugundua kama mtoto wangu anatatizo la usonji na baada ya kubaini nilikwenda mpaka Japan ili kujifunza wenzetu wanafanya nini, nilirudi Tanzania, tatizo ni shule mpaka leo ana miaka tisa.

"Elimu ya mwanzoni haina shida anasoma lakini mtoto anakua, nilimpeleka shule kwa sababu anakuwa mpaka kiti cha shule hakimtoshi hii ni kwa sababu sina pa kumpeleka apate elimu, leo tupo hapa tunajiuliza wazazi wapi wanakwenda?" aliuliza.

Daktari wa watoto mshauri wa magonjwa ya mfumo wa fahamu na ubongo kutoka hospitali ya Saifee, Yusuf Jamnagerwalla, alisema yeye aliwataka wadau wakati wanatafuta ufumbuzi wa tatizo hilo waliangalie kwa upana wake kuanzia ngazi ya chini hadi juu kwa sababu watoto wanakuwa na baadae watahitaji kujitegemea.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alieleza wataalam ndani ya wizara hiyo kuhakikisha wanapata takwimu za watoto.

Mwalimu kutoka Shule ya Msimbazi Mseto kituo cha Usonji, Rukiya Mohammed, alisema matatizo wanayokutana nayo ni upungufu wa walimu ambapo shuleni hapo wapo wanne na inapotokea wanapowapeleka kwenye madarasa ya kawaida ili wachangamane na wenzao wajifunze, baadhi ya walimu husema hawawezi.



Baadhi ya wajasiriamali, wahadhiri na wafanyabiashara, wakijadili miongozo ya moduli ya ufundishaji masomo ya ubunifu na ujasiriamali yanayotarajia kuanza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Tumaini tawi la Dar es Salaam (TUDARCo). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavamizi hifadhi waamriwa kuondoka

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ameutaka uongozi wa Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kusimamia zoezi la wavamizi wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima iliyopo wilayani Kaliua mkoani Tabora wanaondoa mazao yao ambayo yamekomaa.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha TAWA inaendesha shughuli zake za uhifadhi wa mazingira na wanyapori bila kikwazo chochote.

Naibu Waziri huyo alitoa agizo hilo jana katika Kijiji cha Wachawaseme kilichopo eneo la Isawima alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa hadhara.

Alisema kwamba uhifadhi ni muhimu na wenye manufaa makubwa ya taifa na wananchi kwa sasa na vizazi kijacho, hivyo Serikali haiwezi kuacha watu wavamie na kuharibu maeneo hayo.

Mary alisema kwamba kutokana uamuzi wa wakulima kuvamia eneo hilo wanatakiwa kuondoa mazao yao kwa utaraibu maalumu utakaopangwa na Serikali kupitia vibali, ambavyo vitabainisha nini mkulima alichonacho kwenye hifadhi hiyo ili kutambua nani ni nani anaingia kenye hifadhi muda husika.

Alisema serikali haiwezi kuona watu wanavamia hifadhi zilizohifadhi kisheria na kuharibu miundombinu yake kwa sababu ya maslahi ya watu wachache na kuharibu manufaa ya watu wengi nchini.

Aidha Naibu Waziri aliingiza serikali ya mkoa na TAWA kuhakikisha watakapokamilisha kuondoa mazao yao kwenye hifadhi, hakuna mtu yoyote anayeingia ndani ya hifadhi kwa ajili ya shughuli zozote ya kibinadamu zinazokinzana na uhifadhi.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia hifadhi hiyo kuendelezwa kwa shoroba za wanayama na maji kuendelea kutirika hadi Ziwa Tanganyika kwa asilimi 30.

Hata hivyo, aliahidi kutuma wataalam wa kupima mipaka kwa ajili ya kuelimisha wananchi wa vijiji 11 vilivyomo kwenye eneo la Isawima ili kutambua mikapa yote ya kila kijiji na mwisho wa eneo ambalo wananchi hawapaswi kuingia wala kufanya shughuli za kibinadamu.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kaliua, Aloyce Kwezi, alimweleza Naibu waziri huyo kwamba wananchi wa eneo la Isawima ambalo eneo lake kubwa ni hifadhi wanaomba kutambua mikapa yake kwenye eneo lao.

Alisema kutokutambua mipaka hiyo kumesababisha baadhi wa wananchi kuingia eneo la hifadhi na kufanya shughuli za kibinadamu.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, alisema uongozi wa Mkoa hauwezi kuona watu wachache wanatumia fedha zao na kuingia katika eneo hilo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kibindamu.

# IFC wawekeza mabilioni usafiri njia ya mtandao

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya usafiri kwa njia ya mtandao, Bolt imepokea uwekezaji wa Euro 20 milioni kutoka kwa Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC) utakaosaidia kuongeza upatikanaji wa huduma za usafiri katika masoko yanayokua, ikiwamo Tanzania.

Uwekezaji huo ambao unaojumuisha huduma za ushauri kutoka IFC - mshirika wa Benki Ya Dunia, utasaidia Bolt kupanua huduma za usafiri zinazochangia ukuaji wa biashara ndogo ndogo, kukuza fursa za ajira na kuboresha upatikanaji wa huduma za usafiri katika masoko ya Afrika na Ulaya Mashariki.

"Tuna matarajio makubwa ya kushirikiana na IFC kuchangia ujasiriamali, kuwezesha wanawake na kuongeza upatikanaji wa huduma nafuu za usafiri barani Afrika na Ulaya Mashariki. Uwekezaji huu ukijumuishwa na ule tuliopata mwaka jana kutoka Benki ya Uwekezaji Ulaya, inatufanya tuwe na washirika wengi wakubwa wanaoamini umuhimu wa Bolt katika masoko mapya," alisema Markus Villig, Mkurugenzi Mkuu na Mwanzilishi wa Bolt.

Stephanie von Friedeburg, Makamu Mkuu wa Rais wa IFC anayesimamia masuala ya utendaji, alisema: "Teknolojia inaweza na inafaa kufungua fursa mpya za maendeleo endelevu na kuwawezesha wanawake. Uwekezaji wetu katika kampuni ya Bolt unalenga kuwezesha teknolojia kuleta mageuzi chanya katika sekta ya usafiri kwa njia ambazo ni rafiki kwa mazingira, kutoa fursa zaidi za ajira kwa wanawake na kuleta usafiri salama na wa gharama nafuu katika masoko yanayochipuka."

Bolt kwa sasa inapatikana katika nchi saba barani Afrika, huku ikitoa fursa za kipato wa madereva 400,000 katika miji 70 barani.

"Tunaongeza kipato miongoni mwa jamii kwa kuwapa madereva wanaotumia mfumo wetu fursa za kujipatia malipo. Huduma zetu zinaleta mageuzi ya usafiri wa haraka na nafuu kwa mamilioni ya watu wanaoishi mjini," alisema Mkurugenzi wa Bolt Tanzania, Remmy Eseka.

Kwa Tanzania, Bolt inatoa huduma za usafiri wa magari, pikipiki (bodaboda) na pikipiki za miguu mitatu almaarufu bajaji katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza.

# RC aahidi kuinua kilimo cha pamba

**Na Ada Ouko,** SERENGETI

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, ameahidi kuinua zao la pamba mkoani humo hadi kufikia uzalishaji wa tani 50 kwa mwaka.

Malima aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, baada ya kutembelea shamba la mkulima mdogo wa zao hilo ambaye amelima kwa kuzingatia kanuni 10 bora za zao hilo katika Kijiji cha Gusuhi wilayani Serengeti.

Akizungumza kwenye sherehe za siku ya mkulima wa pamba mkoani hapa, Malima alisema mkoa huo umeanza kutekeleza hatua ya kurudisha heshima ya zao hilo, mkoani humo.

Alisema miaka 50 iliyopita zao hilo lililopoteza thamani, na kwamba mipango ya mkoa huo ni kuhakikisha linafufuliwa, na kuwataka maofisa ugani kutoa elimu sahihi ya ulimwaji wa zao hilo kwa wakulima.

''Eneo la Gusuhi lina udongo mzuri uliofanyiwa utafiti na wataalamu, hii imewezesha mbegu bora ya pamba aina za quiton C 577 , C569 kufanya vizuri.

Aidha, alimtaka ofisa kilimo wilayani hapa kuwakusanya wakulima wa zao hilo mkoani hapa ili wafike katika shamba la mkulima huyo wajifunze kanuni na njia alizotumia ili waondokane na kilimo cha mazoea kutoka kilo 150 kwa ekari moja na waweze kufikisha kilo angalao 800 hadi 1500 kwa ekari.

Kwa upande wake ofisa kilimo mkoani hapa, Ruge Kelvin, alisema mafanikio ya mkulima huyo ni matokeo ya kutekeleza agizo la Malima alilotoa Julai mwaka 2020 la kutaka uanzishwaji wa shamba darasa kwenye maeneo yanayolimwa zao hilo mkoani hapa.

Magesa Magabe, ambaye ni ndiye mkulima wa shamba hilo, alisema alianza shughuli hiyo Desemba 4 mwaka jana na kupanda mbegu za Quiton C577, heka nne na Quton C569 za wadau na mbegu nyingine aina ya MO8 ya Bodi ya Pamba.

''Mpaka sasa shamba linaendelea vizuri japo hapo nyuma liliathiriwa kidogo na ukame pamoja na ugonjwa, lakini nilifanikiwa kunyunyizia dawa," alisema.

Nipashe Spotika




WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA MKWAJA MREFU ZAIDI LALIGA UK. 12-13



# WANASOKA WATANO FITI ZAIDI DUNIANI KWA SASA

## ISIKUPITE

BAO la ushindi alilolifunga Trent Alexander-Arnold wakati wakichapa Aston Villa mabao 2-1 juzi, linaifanya Liverpool kuendelea kuwa kinara wa kupata ushindi dakika ya 90 katika ligi hiyo, ikiwa ni mara ya 37 na mara 12 zaidi ya timu yoyote katika Ligi Kuu England.




**LONDON,** England

SOKA la kisasa huwa linahitaji mambo mengi zaidi kutoka kwa wachezaji. Mahitaji makubwa kwa mchezaji ni kuwa fiti kimwili na kiakili ili kuwa na uwezo mkubwa kwa kucheza mpira wa kiwango cha juu.

Huku klabu zikiwa zinahusika kwenye mashindano mbalimbali, pamoja na timu zao za taifa, wachezaji wanatakiwa kuwa kwenye ubora wa hali ya juu kwenye mchezo huu.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao kwa sasa wapo fiti zaidi kwenye klabu zao na timu ya taifa, hawa hapa...

### #5. ZLATAN IBRAHIMOVIC (AC MILAN)

Mmoja wa mastraika bora zaidi kwenye soka la kizazi cha sasa ni Zlatan Ibrahimovic ambaye amedumu kwa muda mrefu mno.

Akiwa na umri wa miaka 39, mchezaji huyo amefurahia nyakati nzuri wakati akicheza kwenye klabu kama Ajax, Inter Milan, AC Milan, Paris Saint-Germain na Manchester United. Baada ya muda mfupi wa kucheza katika klabu ya LA Galaxy kwenye Ligi Kuu Marekani (MLS), raia huyo wa Sweden alijiunga na AC Milan Januari mwaka 2020, na amekuwa mshambuliaji muhimu zaidi huko.

Ibrahimovic amecheza mechi 44 katika mashindano yote kwa AC Milan tangu alipojiunga nayo, akifunga mabao 28. Straika huyo pia atacheza kwenye michuano ya Euro itakayofanyika kuanzia Juni mwaka huu, baada ya kuahirisha kustaafu soka la kimataifa na kurudi tena kwenye kikosi hicho cha Sweden.

### #4. ANDREW ROBERTSON (LIVERPOOL)

Liverpool kwa hakika kabisa imekuwa ina bahati mbaya ya majeruhi msimu huu, lakini mchezaji aliyecheza mara zote kwa kiwango kilekile ni Andrew Robertson.

Wakati Liverpool ilipomsajili kutoka Hull City mwaka 2017 kwa pauni milioni nane, maswali mengi yaliibuka. Misimu minne baadaye, nyota huyo wa kimataifa wa Scotland anachukuliwa kama mmoja wa walinzi bora zaidi wa kushoto kwenye ligi hiyo na mmoja wa wachezaji wasioshuka kiwango pale Liverpool.

Katika umri wake wa miaka 27, amecheza mechi 40 kwenye mashindano yote msimu huu, mara zote akionekana kuwa kiongozi mzuri kwenye safu ya ulinzi kutokana na kukosekana kwa Virgil van Dijk.

### #3. ROMELU LUKAKU (INTER MILAN)

Romelu Lukaku mambo hayakwenda kama yalivyopangwa wakati akicheza pale Manchester United, lakini sasa anaonyesha ubora wake katika kikosi cha kocha, Antonio Conte kule Inter Milan.

Lukaku alijiunga na Inter Milan akitokea Manchester United mwaka 2019 kwa ada iliyoweka rekodi ya klabu ya pauni milioni 67. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amethibitisha ubora wake, akiwa tayari amecheza mechi 86 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo akifunga mabao 60.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, ana rekodi nzuri ya kutokuwa majeruhi, akiwa pia amewahi kuzichezea West Bromwich Albion, Everton na baadaye Manchester United.

### #2. ADAMA TRAORE (WOLVERHAMPTON WANDERERS)

Ni mchezaji mwenye mwili uliojengeka vizuri kwa mazoeni na ana kasi kweli kweli, Adama Traore amekuwa mchezaji muhimu sana kwenye kikosi cha kocha, Nuno Espirito Santo cha Wolverhampton Wanderers.

Ni zao la kituo cha kulelea vipaji cha La Masia, kule Barcelona, na Traore alitumia muda wake kucheza na Aston Villa na Middlesbrough kabla ya kujiunga na Wolverhampton Wanderers mwaka 2018 kwa pauni milioni 18. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa nguzo muhimu zaidi tangu alipojiunga na Wolves.

Nyota huyo wa kimataifa wa Hispania bado hajafunga wala kutoa pasi ya mwisho kwenye ligi msimu huu, licha ya kucheza mechi 28. Amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barcelona na pia kutua Liverpool.

### #1. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS)

Mmoja wa mwanamichezo fiti zaidi duniani ni Cristiano Ronaldo. Akiwa anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea kwenye mchezo wa soka, Ronaldo anaendelea kuonyesha kiwango chake. Akiwa na umri wa miaka 36, ni mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, na bila shaka yoyote ni mchezaji muhimu zaidi kwa Juventus kwenye safu ya ushambuliaji.

Nyota huyo alivunja rekodi nyingi kule Manchester United na Real Madrid kabla ya kujiunga na Juventus na huko nako ameendelea kufanya yake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amecheza mechi 35 kwenye mashindano yote msimu huu na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin, akifunga mabao 31.

# WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA MKWAJA MREFU ZAIDI LALIGA




**MADRID,** Hispania

WACHEZAJI wa mpira wa miguu ni moja kati ya wanamichezo wanaolipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani. Katika miaka ya hivi karibuni, mishahara yao imekuwa mikubwa sana.

**Katika orodha ya Jarida la Forbes, wanamichezo 100 waliokuwa wanalipwa zaidi duniani kwa mwaka 2020, kati ya hao 31 ni wachezaji wa mpira wa miguu, wakipitwa na wachezaji wa Ligi ya Kikapu ya Marekani (NBA), pekee.**

Johan Cruyff aliwahi kunukuliwa akisema - “Kwa nini hamjaifunga klabu tajiri? Kamwe sijawahi kuona begi la fedha linafunga mabao.”

Na hilo huwa na maana kubwa kwa kipindi cha sasa, wakati usajili wa fedha nyingi unaposhindwa kuleta matokeo chanya.

Kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ni Barcelona, Real Madrid na Atletico Madrid pekee ndizo zenye mifuko mikubwa ya kutumia mamilioni ya fedha kwenye soko la usajili.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 ambao walikuwa wanalipwa mshahara mikubwa zaidi kwenye Ligi Kuu Hispania kwa mwaka 2020, twende sasa...

### #10. SERGIO BUSQUETS (FC BARCELONA) – PAUNI 260,000 KWA WIKI

Sergio Busquets, ni mmoja wa wachezaji watano wa Barcelona kwenye orodha hii ya 10. Kiungo huyo alisaini kuongeza mkataba na miamba hao wa Catalunya mwaka 2018, na atakaa hapo Camp Nou hadi kipindi cha majira ya joto mwaka 2023.

Katika mkataba wake wa sasa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, analipwa pauni 260,000 kwa wiki.

### #9. KOKE (ATLETICO MADRID) – PAUNI 270,000 KWA WIKI

Atletico Madrid imeanza kuonyesha nguzo zake za fedha katika miaka ya hivi karibuni na wana wachezaji watatu katika orodha hii ya wachezaji 10.

Nahodha wao, Koke, ambaye mkataba wake wa sasa na klabu hiyo unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2024, analipwa pauni 270,000 kwa wiki.

Kiungo huyo wa Hispania ni mmoja kati ya wachezaji wanne ambao wamelipa fadhila vizuri katika klabu yake hiyo ya utotoni kwenye kizazi chake. Atatimiza umri wa miaka 29 Januari mwakani na amejifunga kwa muda mrefu katika klabu hiyo, kwani si wa kuondoka leo au kesho.

### #8. DIEGO COSTA (ATLETICO MADRID) – PAUNI 270,000 KWA WIKI

Diego Costa anaungana na Koke kwenye orodha hii akiwa na mshahara wa pauni 270,000 kwa wiki katika klabu hiyo aliyojiunga nayo Januari 2018, baada ya kumaliza uhamisho wake wa pauni milioni 58 kutoka Chelsea.

Aliondoka hapo mwaka 2014 kama mmoja wa mastraika bora kabisa duniani, lakini aliporudi tena hapo katika uwanja wa Wanda Metropolitano mwaka 2018, alipoteza uwezo wake wa kufunga. Na kwa sasa hayupo tena klabuni hapo.

Mkataba wake umesitishwa na nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, anatarajia kutafuta timu nyingine ya kuichezea msimu ujao.

### #7. ANTOINE GRIEZMANN - (FC BARCELONA) – PAUNI 346,000 KWA WIKI

Antoine Griezmann, mchezaji wa zamani wa Atletico ambaye alisubiri kwa muda mrefu kujiunga na Barcelona kipindi cha majira ya joto, aliripotiwa kukubali kupunguziwa mshahara na sasa anachukua pauni 346,000 kwa wiki.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2024 na hivyo ana muda mrefu wa kuthibitisha thamani yake ya pauni milioni 107 aliyosajiliwa nayo wakati akitoka Atletico na kutua hapo ‘Blaugrana’.

### #6 GARETH BALE (REAL MADRID) – PAUNI 350,000 KWA WIKI

Gareth Bale awali alikuwa anachukuliwa kama mmoja wa wacheza bora wachache duniani katika miaka yake michache ya mwanzo pale Real Madrid, akiwa anacheza kwa kiwango bora kabisa kwa kushirikiana na Cristiano Ronaldo na Karim Benzema.

Uhusiano wake wa sasa na Zinedine Zidane ukamfanya kuwa kwenye wakati mgumu na kupelekwa kwa mkopo kule Tottenham Hotspur.

Raia huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 31, kwa sasa mshahara wake ni pauni 350,000 kwa wiki.

### #5. JAN OBLAK (ATLETICO MADRID) – PAUNI 350,000 KWA WIKI

Kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili 2019 hadi Septemba 2019, golikipa namba moja wa Atletico Madrid, Jan Oblak alikuwa kipa anayelipwa mshahara mkubwa zaidi duniani, shukrani kwa kusaini mkataba mpya ambao utamuweka hapo hadi kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2023.

Oblak amejithibitisha yeye mwenyewe kama mmoja wa magolikipa bora kabisa duniani kwa kulinda vizuri lango lake na anabeba nyumbani kiasi cha pauni 350,000 kwa wiki.

### #4. FRENKIE DE JONG (FC BARCELONA) – PAUNI 360,000 KWA WIKI

Mchezaji kijana zaidi kwenye orodha hii, licha ya ada yake ya pauni milioni 65.3 aliyosajiliwa nayo wakati akitoka Barcelona kutoka Ajax, Frenkie de Jong analipwa mshahara wa pauni 360,000 kwa wiki.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alisaini mkataba wa miaka mitano na miamba hao wa soka la Hispania, ambao utamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2024.

### #3. EDEN HAZARD (REAL MADRID) – PAUNI 400,000 KWA WIKI

Eden Hazard ni mchezaji wa pili kuwapo kwenye orodha hii akiwa anachukua mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki, ikiwa ni mara mbili zaidi ya ule aliokuwa anachukua kule Chelsea.

Winga huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara tangu alipotua hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu kwa ada ya pauni milioni 88.5.

Bahati nzuri kwa upande wake alibeba taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwenye msimu wake wa kwanza, na kuna matumaini makubwa kwamba anaweza kuwa fiti kwa ajili ya msimu ujao.

### #2. LUIS SUAREZ (FC BARCELONA) – PAUNI 405,000 KWA WIKI

Mchezaji wa zamani wa Barcrelona, Luis Suarez, ambaye kwa sasa anacheza kule Atletico Madrid, anachukua kiasi cha pauni 405,000 kwa wiki.

Baada ya kufanya vizuri zaidi akiwa na Barcelona akishirikiana vizuri sana na Lionel Messi, Suarez sasa anatamba na Atletico

### #1. LIONEL MESSI (FC BARCELONA) – PAUNI 1,224,000 KWA WIKI

Sio jambo la kushangaza kumuona Lionel Messi akiongoza kwenye orodha hii ya wachezaji wanaolipwa mkwanja mrefu zaidi kwenye LaLiga.

Mshahara wake wa sasa utakumbukwa kwa siku za usoni kwa sababu ni mchezaji bora wa wakati wote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ndiye mwanasoka pekee duniani ambaye mshahara wake wa wiki una namba saba kwa maana pauni 1,224,000, ikiwa ni mara mbili zaidi ya anacholipwa mchezaji mwenzake wa zamani, Neymar kule PSG.

Msimu uliopita, ndio ulikuwa msimu pekee ambao mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alimaliza bila taji lolote.

## Nukuu

“Toto la Kulia’, ndio, kwa sababu Ronaldo alikuwa tayari anapenda kushinda kama anavyopenda leo. Na wakati aliposhindwa na wakati watoto wengine hawakumpasia mpira alikuwa akilia,” **Ricardo Santos, ambaye alishiriki chumba kimoja cha kubadilishia nguo na Cristiano Ronaldo wakati wakicheza pamoja CF Andorinha, akielezea jina la utani la utotoni la CR7.**



“Sikuamini bodi ambayo ilikuwa kwenye klabu wakati huo na baadaye, silika yangu ilithibitishwa kuwa sawa, kama nilikuwa wa kwanza kusema, watu walidhani nilikuwa mwendawazimu kabisa; kwa kweli mimi ni mwendawazimu kidogo, lakini kwa njia nzuri,” **Beki wa pembeni wa Brazil, Dani Alves akiilaumu Bodi ya Barcelona kuwa chanzo cha yeye kuondoka Camp Nou mwaka 2016.**



“Kuna mechi chache zimebakia ligi kumalizika, nafikiri ligi hii inakwenda kuwa na ushindani mkubwa, kwa sababu bado ushindani ni mkubwa. Tunatakiwa kucheza kila mchezo kama fainali,” **mshambuliaji wa Real Madrid, Mfaransa Kazim Benzema.**



# YANGA 'ILIVYOSHONA' SARE 9 LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

JUZI ilikuwa ni sare ya tisa kwa Yanga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21. Ni baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC FC, mechi ikichezwa saa 1:00 usiku, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Matokeo hayo yanaifanya Yanga kuwa moja kati ya timu zenye sare nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa, ikishika nafasi ya nne. Polisi Tanzania ndiyo vinara wa sare ikiwa imezikunya 13, Mbeya City ikiwa nafasi ya pili na sare zake 12, maafande wa Prisons wakishika nafasi ya tatu wakiwa na sare 10.**

Yanga inakamata nafasi ya nne ikiwa na sare tisa, pamoja na timu za Coastal Union na Gwambina ambazo zote zina idadi hiyo ya sare. Ilikuwa ni sare ya pili mfululizo baada ya ile ya Machi 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha dhidi ya Polisi Tanzania.

Ilipata sare hiyo, baada ya kutoka kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union, Machi 4, Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga. Pamoja na kwamba bado inaongoza Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 51, ikicheza mechi 24, Yanga iko kwenye presha kubwa kutoka kwa timu za Azam na Simba.

Imeizidi Simba pointi tano tu, huku ikiwa imecheza mechi nne zaidi, lakini matokeo mabaya ya hivi karibuni yameifanya kupata joto pia kutoka kwa Azam ambayo nayo imefikisha pointi 47, tofauti ya pointi nne tu.

Pamoja na kwamba imecheza michezo 25, mechi moja zaidi ya Wanajwangwani hao, lakini Yanga kama itaendelea na mwenendo huo, basi Azam ambayo kwa sasa inashika nafasi ya pili, inaweza kabisa ikakaa juu yake hivi karibuni.

Makala haya yamekukusanyia matokeo yote ya sare tisa za Yanga ambayo msimu huu imetajwa wakati huu ikipambana kusaka ubingwa wa Tanzania Bara iliyoukosa kwa misimu mitatu mfululizo, shuka nayo sasa...



Straika wa Yanga, Fiston Abdoulrazak, akipambana na beki wa KMC, Vicent Andrew 'Dante', (Kulia) kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

### #1. YANGA 1-1 PRISONS

Yanga ilianza 'kushona' sare zake mapema tu, kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Septemba 6, mwaka jana ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Maafande wa Prisons kutoka Mbeya. Ilikuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Lambart Subianka akianza kuiandikia Prisons bao dakika ya saba, lakini Michael Sarpong akasawazisha dakika ya 18.

### #2. GWAMBINA 0-0 YANGA

Ni Novemba 3, mwaka jana, Yanga ikienda kwenye Uwanja wa Gwambina, Misungwi, Mwanza, na kuambulia suluhu dhidi ya wenyeji Gwambina FC, ikawa ni sare ya pili kwao kwenye Ligi Kuu.

### #3. YANGA 1-1 SIMBA

Hii ni mechi ya watani wa jadi iliyochezwa Novemba 7, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikiwa mwenyeji.

Ilionekana kama Yanga ingeondoka na ushindi kwenye mechi hiyo baada ya Sarpong kufunga bao kwa mkwaju wa penalti dakika ya 31. Lakini zikiwa zimebaki dakika tano kabla mwamuzi kupuliza kipenga cha mwisho, beki Joash Onyango aliisawazishia Simba na kutoka sare ya bao 1-1, ikiwa ni ya tatu kwa Yanga.

### #4. YANGA 1-1 NAMUNGO

Muangola Carlos Carlinhos alianza kuiandikia Yanga bao dakika ya 12 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Novemba 22, mwaka jana. Dakika tatu tu baadaye, Mghana, Steven Sey aliisawazishia Namungo, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 na kuhesabika kuwa ni sare ya nne kwa timu hiyo msimu huu. Hapa utaona kuwa mwezi Novemba Yanga ilipata sare tatu.

### #5. PRISONS 1-1 YANGA

Kwa mara nyingine tena, Yanga ilikutana na Maafande wa Prisons kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara. Ilikuwa ni Desemba 31, mwaka jana Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga. Kama ilivyokuwa mechi ya mzunguko wa kwanza, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Jumanne El Fadhili akiifungia Prisons bao dakika ya 51, Saido Ntibazonkiza akisawazisha dakika ya 75.

### #6. MBEYA CITY 1-1 YANGA

Yanga ilikwenda kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya kucheza na wenyeji Mbeya City, ikapata sare yake ya sita kwenye Ligi Kuu, Februari 13, mwaka huu. Deus Kaseke alianza kuiandikia Yanga bao dakika tano kabla ya mechi kumalizika, lakini Pastory Athanas alisawazisha kwa mkwaju wa penalti dakika nne za nyongeza.

### #7. YANGA 3-3 KAGERA SUGAR

Bonge la mechi lilichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mashabiki wakishuhudia mabao sita yakifungwa kwenye mechi moja. Yanga iliikaribisha Kagera Sugar na kufungana mabao 3-3, Februari 17, mwaka huu.

Mabao ya Yanga yalifungwa na Tuisila Kisinda dakika ya 14, Deus Kaseke 29 na Mukoko Tonombe 61, Peter Mwalyanzi akiifungia Kagera Sugar dakika ya 11, Hasan Mwaterema dakika ya 25 na Yusuph Mhilu dakika ya 61.

### #8. POLISI 1-1 YANGA

Yanga ilipata sare ya nane kwenye Ligi Kuu, Uwanja wa Sheik Amri Abeid jijini Arusha, ilipolazimisha kufungana bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania. Fiston Abdoulrazak aliipatia Yanga bao, ambalo lilisawazishwa dakika ya 90 na Pius Buswita, mechi ikichezwa Machi 7, mwaka huu.

### #9. YANGA 1-1 KMC

David Bryson alianza kuifungia KMC bao dakika ya 29, lakini dakika mbili tu baada ya mapumziko, Yacouba Sogne aliisawazishia na kuzifanya timu hizo kutoka sare ya 1-1, mechi ikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni sare ya tisa kwa Yanga ambazo zinaonekana kutishia uwezekano wa kuukosa ubingwa msimu huu kwa mara nyingine tena.

## JE, WAJUA?



KATIKA hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kwenye Kundi A, Simba imemaliza ikiwa kinara baada ya kujikusanyia pointi 13 ikifuatiwa na Al Ahly ya Misri iliyovuna pointi 11. Kwa mantiki hiyo hatua ya robo fainali Simba sasa inaweza kupangwa kukutana na CR Belouizdad ya Algeria, Kaizer Chiefs (Afrika Kusini) ama MC Alger (Algeria), wakati Al Ahly yenyewe inaweza kukutana na Wydad Casablanca ya Morocco, ES Tunis (Tunisia) ama Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.



# Asilimia 45 ya vifo vinatokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa zaidi ya asilimia 45 ya vifo nchini vinatokana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanazuilika kwa asilimia 80 hadi 90.

Hata hivyo, idadi hiyo ya vifo ikikadiriwa kufikia asilimia 60 ifikapo 2025, endapo Watanzania hawatabadili mtindo wa maisha yao kwenye mlo na ufanyaji mazoezi.

Mwenyekiti wa Shirikisho la vyama vya magonjwa yasiyoambukiza (TANCDA), Prof. Kaushik Ramaiya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye semina iliyoandaliwa na Shirikisho hilo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Alisema licha ya magonjwa yasiyoambukiza kuchangia asilimia kubwa ya vifo lakini yanazuilika kwa zaidi ya asilimia 80, ikiwa Watanzania watabadili tabia katika mlo, kufanya mazoezi na kuacha matumizi ya vilevi. Prof. Ramaiya alibainisha kuwa magonjwa hayo gharama za matibabu ni kubwa na kushauri serikali iangalie uwezekano wa Bima ya afya kwa watu wote.

"Kinga ni bora kuliko tiba tujikite kwenye kutoa elimu katika ngazi zote za juu ya ufanyaji mazoezi, lishe sahihi na kuacha matumizi ya vilevi, gharama ni kubwa za matibabu ni vyema kukinga," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Stanslaus Nyongo, alisema zinahitajika mbinu na mikakati madhubuti ili kukabiliana na magonjwa hayo yanayochangia vifo vingi.

"Tumeona kuna vifo vingi vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukizi, kwa mfano asilimia 100 ya vifo vinavyosababishwa na magonjwa mbalimbali asilimia 30.6 inasababishwa na magonjwa ya moyo ambayo si ya kuambukizwa,"alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa saratani asilimia zaidi 15 ya vifo husababishwa na magonjwa hayo na vifo vinavyotokana na virusi vya UKIMWI ni asilimia 4.2 tu.

Alisema tatizo hilo ni kubwa linahitaji hatua pekee za kuchukua. "Tumeona Wizara ya Afya inashughulikia ununuzi wa vifaa tiba na dawa na kutibu wagonjwa lakini tunawatibu katika hatua ya pili ya magonjwa ile hatua ya mwanzo haipewi kipaumbele,"alisema.



Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, George Masaju, akizungumza na wazazi na wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari ya Central ya Dodoma, kwenye mahafali yaliyofanyika shuleni hapo jana, kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Hashimu Swaib. **PICHA PETER MKWAVILA.**

# TAMISEMI yapewa maagizo matatu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameliagiza Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo, mambo matatu ya kushughulikia ikiwamo upungufu wa watumishi kwenye baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa.

Pia, kusimamia masuala ya mapato kwenye halmashauri huku akisema zilizopata hati safi baadhi zimefichwa na ubadhirifu na ufisadi wa fedha za umma.

Akifungua kikao hicho jana, Waziri Ummy alisema ofisi yake ina kazi ya kufanya kuhakikisha inasimamia mamlaka za serikali za mitaa kwenye masuala ya mapato.

"Kusimamia mapato na matumizi, kusimamia masuala ya mgawanyo wa fedha za maendeleo," alisema.

Kuhusu uhaba wa watumishi, Waziri huyo alisema kuna uhaba mkubwa wa watumishi kwenye mamlaka hizo na kumshukuru kukubali kutoa ajira za kuziba pengo la walimu 6,000 ambao wamestaa, wameacha kazi au kufariki.

"Wakati tunasherehekea mafanikio yaliyopatikana lakini tuangalie na suala la uhaba wa watumishi kwenye baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa, Katibu Mkuu baraza lako litaona kama moja ya mapendekezo kuangalia tena mgawanyo wa watumishi kwenye halmashauri," alisema.

Aliwahimiza kufanya kazi kwa tija, ufanisi, umoja, mshikamano na uwajibikaji, kutimiza wajibu wao katika nafasi walizonazo bila ya kujali cheo wala daraja na kuzingatia maadili, weledi na ubunifu katika kazi.

Waziri huyo alisema katika utekelezaji wa majukumu yao ni muhimu kuhakikisha linakuwa na uwiano kati ya tija na maslahi.

"Ili kupata matokeo mema ni vyema tukaweka uwiano kati ya tija na maslahi na tukumbuke utendaji bora wa kazi unaongeza tija, na ili tufanikiwe ni lazima tujitathmini, umekuja kazini asubuhi na jioni unaondoka jiulize kwa siku husika umefanya nini,"alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, alisema baraza hilo linalenga kuongeza tija na uwajibikaji mahala pa kazi na limekutana kwa ajili ya kujadili na kupitisha bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

# Waziri Jafo awapa angalizo w'biashara chuma chakavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amewataka wafanyabiashara wa vyuma chakavu kufanya biashara hiyo kwa kuzingatia sheria za nchi na kujiepusha na uharibifu wa miundombinu.

Waziri Jafo alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kongamano la wanafunzi wa vyuo na shule za sekondari lilioenda sambamba na upandaji miti ili kuifanya Dodoma ya kijani lililoandaliwa na Chama cha washerehеshaji nchini (Kisima cha mafanikio).

Alisema wafanyabiashara hao wanapaswa kuzingatia sheria ya mazingira na si kukata vyuma ovyo ambavyo vitasababishwa uharibifu wa miundombinu.

"Naomba fanyeni biashara yenu kwa kufuata sheria na sio kung'oa vyuma ovyo mnavyovikuta na kusababisha uchafuzi wa mazingira,"alisema Jafo.

Kuhusu upandaji miti, Waziri Jafo alisema ataanzisha mashindano ya kupanda miti katika taasisi,vyuo na shule ikiwemo kutoa zawadi ili kuhamasisha utunzaji mazingira na kuifanya Dodoma na mikoa mingine kuwa ya kijani.

"Natarajia kuanzisha mashindano ya utunzaji miti katika taasisi mbalimbali lengo ni kuhamasisha jamii ijue wajibu wa utunzaji wa mazingira," alisema Jafo.








Watoto wakikatisha mitaa ya Jiji la Mbeya, baada ya kutoka kutafuta kuni nje kidogo ya mji, ikiwa ni sehemu ya wajibu wao kuwasaidia wazazi siku za wikiendi. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Wanawake viongozi wapewa jukumu kupambana na ukatili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIONGOZI wanawake wamehamasishwa kuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwenye nafasi walizonazo ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Miongoni mwa vitendo hivyo vimetajwa ni vipigo, ubakaji na rushwa ya ngono. Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa vikundi vya taarifa na maarifa vilivyoanzishwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, wakati akiwajengea uwezo wanawake kuwa viongozi bora kutetea maslahi ya wenzao kwenye Kijiji cha Iwalanje Kata ya Ijombe

Alisema miongoni mwa masuala yanayopaswa kupigiwa kelele ni suala la ukatili wa kijinsia na mfumo dume, ambao unachangia wanawake kushindwa kugombea nafasi mbalimbali kutokana na fedheha zinazotolewa na makundi mbalimbali ya watu kwamba hawana uwezo wa kuongoza.

"Bado tuna kazi ya kuwahamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kufikia ile 50 kwa 50 kwenye nafasi zote, kwa hali iliyopo sasa kuna gap (upungufu) mkubwa, tunahitaji kukaba hizo nafasi na tutafanikiwa endapo tutashikamana na kupendana," alisema Mlowezi.

Alisema jamii inapaswa kutambua mchango wa mwanamke kuanzia ngazi ya familia hadi taifa, kutokana na mambo mazuri wanafanya katika k utekeleza majukumu yao kama kutunza familia, uadilifu na kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo.

Aligusia suala ya malezi kwa watoto wa kike, alivishauri vituo vya taarifa na maarifa kuhamasisha klabu za wanafunzi shule za msingi na sekondari wilayani Mbeya ili vijengewe uwezo namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ili kutimiza ndoto zao kupitia masomo.

Alisema baadhi ya shule zina klabu za kupinga ukatili wa kijinsia, lakini nyingine bado, hivyo vituo vya taarifa na maarifa vina jukumu la kuhamasisha ili kutokomeza kabisa unyanyasaji kwa watoto wa kike kwa kujengewa uwezo namna ya kukabiliana na vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Iwalanje, Geofrey Mwande, alisema miongoni mwa mambo yanayochangia wanawake kudharauliwa ni unywaji wa pombe kupita kiasi na kusababisha kufanya matendo yasiyofaa akilewa.

Alisema kwa mazingira hayo yanachangia kushusha heshima na anapogombea watu hutunza kumbukumbu na kuanza kumkashifu.

Aliwashauri wanawake kulinda utu na heshima yao ili kutonyooshewa vidole pale wanapojitokeza kugombea nafasi za uongozi kwa lengo la kutetea maslahi yao.

# W'biashara sokoni waomba mazingira bora ulipaji kodi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa masoko ya Sido na Mwanjelwa jijini Mbeya, wameiomba serikali kutekeleza kwa vitendo suala la kuboresha mazingira ya ulipaji wa kodi ili waendelee kufanya kazi kwa uhuru.

Walitoa ombi hilo jana wakati wakizungumza na Nipashe juu ya hali ya kibiashara tangu Rais Samia Suluhu Hassan kutoa maelekezo ya kuboresha mazingira kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Atupele Mwinuka alisema kauli ya Rais Samia imeleta matumaini mapya kwa wafanyabiashara wanaosubiri ni kuona utekelezaji wa maelekezo hayo kwa watendaji wake.

Alisema awali kulikuwa na utitiri wa kodi na kutolewa lugha zisizofaa kutoka kwa maofisa wanaokusanya kodi hali iliyosababisha wakati mwingine kufunga biashara zao au kukimbia walipowaona.

"Kwa kweli tulijitahidi kufanya kazi kwenye mazingira magumu mno, tulikuwa tunanyonywa, kila mtu alikuwa anabuni kodi yake, walikuwa wanapishana tu, tumepata nafuu baada ya kauli ya Rais tunachoomba sasa ni utekelezaji wake ili tuweze kulipa kodi halali," alisema Mwinuka.

Salome Angumbwike alisema licha ya kuletewa utitiri wa kodi, lakini kauli za maofisa wakusanya kodi hazikuwa nzuri, alidai hawakuwa na kauli ya kiungwana ambayo inaonyesha wanajenga Tanzania moja, bali walitumia ubabe na vitisho kudai.

Alisema kipindi cha Janga la Corona kilikuwa mtihani kwake kwa sababu ya kukosa wateja, hali iliyomlazimu kufunga biashara, lakini aliendelea kusumbuliwa na wakusanya kodi.

Licha ya wafanyabiashara hao kuomba utekelezaji wa agizo la Rais Samia kuweka mazingira mazuri ya kulipa kodi, pia madereva bajaji katika jijini hilo wamepaza sauti zao kuiomba serikali kuondoa baadhi ya ushuru wakidai unawaumiza.

Gaspar Kayuni, dereva bajaji jijini Mbeya, alisema Halmashauri ya jiji hilo imepandisha ushuru kutoka Sh. 500 kuingia kwenye stendi ya Kabwe hadi Sh.1,500.

Alisema kulingana na hali ya kiuchumi, kiwango hicho ni kikubwa, hivyo wanaomba uongozi wa Jiji kupunguza kiwango hicho kwa sababu kinawaumiza.

# Wanawake, vijana wakwama viwanda usindikaji vyakula

**Na Grace Mwakalinga,** BUSOKELO

VIKUNDI vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanaonufaika na mikopo ya asilimia 10 za mapato ya ndani katika Halmashauri ya Busokelo, vinashindwa kuanzisha viwanda vya kusindika bidhaa za vyakula.

Inadaiwa kwamba sababu ya kukwama ni urasimu wa taasisi zinazosimamia shughuli hizo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Agnes Elikunda, aliyasema hayo juzi wakati wa kutoa mkopo wa Sh. milioni 133 kwa vikundi 25 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo ilikabidhiwa na Mbunge wa Jimbo la Busokelo, Atupele Mwakibete.

Alisema vikundi hivyo huwa vinahitaji kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika vyakula, lakini kutokana na urasimu wa taasisi hizo wenye vikundi huwa wanakata tamaa na kuamua kufanya shughuli zingine.

"Vikundi vingi havina miradi yenye mwelekeo wa viwanda kutokana na tatizo la urasimu ambao vinakutana nao kwa wahusika wanaosajili shughuli hizo, lakini tunaendelea kutoa elimu na kuhamasisha ili waendelee kupambana," alisema Agnes.

Aidha alisema vikundi vingi vimekuwa vikiomba mikopo hiyo, lakini vinakosa sifa za kukopesheka hasa vijana na watu wenye ulemavu na kwamba vikundi vya wanawake havina tatizo kubwa.

Alisema vikundi vya vijana huwa havikidhi vigezo vya kukopeshwa fedha hizo kutokana na wengi kuwa na umri wa zaidi ya miaka 35 unaohitajika kisheria, na kwamba wenye ulemavu huwa wanakosa sifa kwa sababu wanaunda vikundi lakini wanakuwa hawafahamiani vizuri.

Mbunge wa Busokelo Mwakibete aliwataka wanufaika wa mikopo hiyo kuirejesha kwa wakati ili vikundi vingine vinufaike kama ambavyo inatakiwa kwa mujibu wa sheria. Alisema kwa vikundi vya vijana ambavyo havinufaiki na mikopo hiyo kwa sababu ya kigezo cha umri, wataunganishwa na taasisi za fedha ili wakopeshwe huko na waendeshe shughuli zao kwa faida na kuboresha maisha yao.

Alisema vilevile zipo fedha ambazo zinatoka katika Mfuko wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na zinazotoka kwenye mashirika ya kimataifa ambazo zinatakiwa zinufaishe vikundi hivyo, lakini Halmashauri hiyo haijawahi kunufaika nazo.

Aliongeza kuwa fedha hizo endapo wanufaika watazitumia vizuri zitawafanya kuwa matajiri na endapo watazitumia hovyo wataendelea kuwa maskini.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo waliishukuru Serikali kwa kuanzisha utaratibu huo kwa madai kuwa umewasaidia kuboresha maisha yao kwa kujiinua kiuchumi.

Mmoja wa wanufaika hao, Ikupasya Mwakasege, alisema kutokana na mikopo hiyo ameweza hata kusomesha watoto wake ambao mmojawapo anasoma Chuo Kikuu, na kwamba ana biashara ambayo inamuwezesha kuendesha maisha yake na kurejesha mikopo.



# Shule zenye ufaulu mdogo kufuatiliwa

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Elimu ya Sekondari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi Issa, amewataka maofisa elimu , walimu pamoja na kamati za shule, kuzifuatilia shule zenye ufaulu wa chini ili kuwandaa vizuri kwa ajili ya mitihani ijayo.

Alitoa melekezo hayo katika shule ya Kitongani Mkoa wa Kusini Unguja wakati wa mkutano maalum na watendaji hao juu ya namna ya kufanya kazi kwa pamoja na Idara za TAMISEMI katika kuleta maendeleo ya elimu.

Alisema kuna tatizo la ufaulu mdogo wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali hasa katika madarasa yenye mitihani ya Taifa ambayo ni kidato pili, kidato cha nne na kidato cha sita, huku wanafunzi wa darasa la nne wakionekana kutokuwa na msingi mzuri kutokana na matokeo yao kipindi cha mitihani .

Alisema ni vyema kuandaa mikakati itakayopatikoa ufumbuzi wa tatizo hilo kwa kutoangalia tu katika madarasa yenye mitihani bali kuanzia katika ngazi za madara ya chini kwa kuwandaa vyema kupitia shule hizo ambazo mara nyingi ufaulu wao sio wa kuridhisha.

"Ni vyema katika kutatua changamoto hii tukaanzia madarasa ya chini, kwa sababu mtoto anapoandaliwa vizuri katika msingi basi hata akifika ngazi ya kidato atafanya vizuri, hivyo tujikite katika ngazi za chini huku tukiangalia na ngazi hizi za juu,"alisema.

Aidha, aliwasisitiza maofisa na walimu kusimamia majukumu yao ipasavyo hasa katika suala la utoro wa wanafunzi pamoja na usafi katika maeneo ya shule pamoja na mavazi ya wanafunzi ili wawe na mwonekano mzuri wanapokuwa shuleni.

Pia aliwataka walimu kuwa na nidhamu katika kuzungumza kuandika hata katika michezo ili wanafunzi wadumishenidhamu.

Mapema akifungua mkutano huo, Naibu Katibu Tawala za Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ, Dk. Haji Salim Khamis, alizitaka tasisi za elimu zilizogatuliwa kufanya kazi kwa pamoja kama sekta nyingine zinazofanya kazi vizuri zikiwamo za afya na sekta za ardhi ili kuhakikisha lengo la kutoa elimu bora kwa watoto wao linafikiwa kwa maendeleo ya nchi. Alisisitiza wasimaizi wote wanaohusika na elimu kusimamia vizuri kwani hivi sasa kumeonekana kuwapo na usimamizi dhaifu, hali inayochangia kushuka kwa ufaulu kwa watoto.



Mkurugenzi Idara ya Elimu Sekondari, Asya Iddi Issa, akizungumza na maofisa elimu (hawapo pichani) katika Shule ya Kitogani, Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Elimu yatakiwa mpango wa kurekebisha tabia za watoto

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja, Salum Kassim Ali, amesema elimu zaidi inahitajika kwa jamii juu ya mpango wa marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria.

Amesema watoto hao wamo katika hatari zaidi ya kukumbana na vishawishi vinavyopelekea kufanya matendo maovu,

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na maofisa ustawi wa jamii, waratibu na watendaji wa mradi wa kurekebisha tabia kwa watoto wanaokizana na sheria wakati akifungua mafunzo ya siku tano katika ofisi ya mkoa huo iliyopo Tunguu.

Alisema licha ya serikali na jumuiya mbalimbali kuendelea na juhudi za kuwanusuru watoto na majanga, bado jamii haina uelewa wa kutosha juu ya masuala ya hifadhi ya mtoto wanaokinzana na sheria, hivyo ni vyema kwa wadau hao kuchukua juhudi za makusudi za kuelimisha jamii juu ya masuala hayo kuhakikisha watoto wanabaki salama na kuwa wenye maadili mema.

Alisema lengo la serikali kushirikiana na mashirika yanayowahudumia watoto ni kuhakikisha jamii inapata elimu na kuhusiana na masuala hayo ili watoto wajiepushe na makosa mbalimbali yakiwamo ya wizi, uvutaji wa madawa ya kulevya na udhalilishaji.

"Licha ya kuendelea kutoa elimu juu ya masuala hayo, ushirikiano wa pamoja unahitajika kati ya wazazi, walezi na watoto wenyewe ili kuona namna gani tunaweza kulitatua tatizo, kulipunguza ama kulimaliza kabisa." alisema.

Alisema Wazazi na jamii wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kupigania watoto wao ili wakue katika malezi mema na kuwakinga na malezi haya ambayo hupelekea kufanya vitendo viovu wakiwa katika umri mdogo.

Nao washiriki wa mafunzo hayo wamesema uwapo kwa sheria ya mtoto ya mwaka 2011 no 6 kifungu cha 19 umeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kurekebisha tabia za watoto.

Washiriki hao ameishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha vituo vya malezi kwa watoto katika ngazi za mikoa yote ya Zanzibar ili kusaidia kuondokana na msongamano wa watoto katika kituo kilichopo sasa katika mkoa wa Mjini Magharibi kwa Unguja pekee.

Nae mratibu wa kurekebisha tabia kitaifa, Diwani Maulid Diwani, alisema tangu kuazishwa kwa mradi huu mwaka 2015 kumeweza kupokea watoto zaidi ya 200 na kufanikiwa kurekebisha tabia watoto zaidi ya 100.

## Wajasiriamali bidhaa za utalii wapewa ushauri

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wanaobuni bidhaa mbalimbali ambazo zinawavutia hasa watalii, wametakiwa kujiendeleza wanapopata nafasi za kusaidiwa na wawekezaji wa sekta hiyo.

Hayo yameelezwa na Meneja wa Mgahawa wa Beach House, Afshan Jivraj, katika monyesho ya bidhaa za kitalii zinazobuniwa na wajasiriamali wa Zanzibar juzi.

Alisema mgahawa huo umeamua kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupitia miradi mbalimbali kwa lengo la kuwanyanyua ili baadae waje kuwa wajasiriamali wakubwa na wenye mafanikio hususani katika kipindi hiki ambacho dunia imekumbwa na janga la Corona na kuathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Alisema mbali na miradi mingine ya kijamii wanayoifanya, pia wanavinyanyua vikundi vya ujasiriamali ambao wengi wao soko la bidhaa zao zinategemea zaidi watalii wanaokuja nchini.

Alisema katika kipindi cha mlipuko wa virusi vya Corona wajasiriamali wengi ambao wanabuni bidhaa hizo walishindwa kufanya kazi zao kutokana na janga hilo hali iliyopelekea baadhi ya mataifa kutoruhusu raia wao kusafiri. "Tunajua Corona ilivyoathiri kwa kiasi kikubwa, si sekta tu ya utalii tu bali karibu sekta zote, hivyo wajasiriamali hawa kwa kuwasaidia tumeona tuwaandalie maonyesho maalum ambayo yanashirikisha wageni na wenyeji ili wapate kuuza bidhaa zao ," alisema.

Mjasiriamali anayejishughulisha na uchoraji wa maua katika vitezo, machanuo, nyungo pamoja na picha za mapambo, Jamila Mzee, alisema katika kipindi cha Corona walishindwa kufanya biashara zao kutokana na kutokuwapo watalii wanao kuja nchini.

Alisema biashara yake inategemea zaidi watalii, hivyo kitendo cha mataifa mengi kutoruhusu raia wao kusafiri kilipelekea kushindwa kuuza bidhaa hizo na badala yake kukosa wateja wa uhakika.

Alisema mbali na kukosa wateja wa uhakika, athari nyingine ilitokana na kutopatikana kwa baadhi ya vifaa, ambavyo anatumia kutengeza bidhaa zake ikiwamo rangi.

Wajasiriamali hao wanasaidiwa kujitangaza kupitia Hoteli ya Park Hyatt kwa kuwaandalia kazi mbalimbali ambazo zinawashirikisha wageni wa kitalii ili kuuza biashara zao na kujitangaza.

HABARI KITAIFA

# Wavuvi wakwama soko la nje bidhaa za uvuvi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAFANYABIASHARA wa mazao ya uvuvi katika mwalo wa Katonga na Kibirizi Manispaa ya Kigoma kwenda nchi jirani kama Congo, Burundi na Rwanda wamelalamikia biashara hiyo kufanya vibaya tangu mwaka 2020.

Wafanyabiashara hao wakizungumza na Nipashe juu ya mwenendo wa kibiashara, wamesema kwa kipindi kirefu hali imekuwa mbaya na kuwafanya wakose mitaji na baadhi yao kushindwa kurejesha madeni waliyokopa ili kukuza biashara zao.

Hamza Juma, mfanyabiashara katika Mwalo wa Katonga, alisema hali ilianza kusuasua tangu mwaka jana kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona wakati ambapo nchi zilibadilisha utaratibu wa kuingia na kutoka ikiwamo watu kuwekewa karantini kwa siku 14.

Alieleza tangu kipindi hicho hadi sasa soko la nje sio la kueleweka tena, kutokana na baadhi ya nchi kama Burundi kuwa na masharti ya kujikinga na janga la ugonjwa wa Corona, ambayo si rafiki kwa mwingiliano wa kibiashara.

Mwenyekiti wa chama cha wavuvi Mkoa wa Kigoma, Fransis John, akielezea kwa ujumla hali hiyo alisema wengi wa watu wanaotegemea biashara ya mazao ya uvuvi kwenda nje kwa sasa hawana mitaji tena kutokana na kuzorota kwa biashara hiyo, na kuiomba serikali kutafuta namna ya kuwasaidia.

Kwa upande wake Ofisa Biashara Kigoma Manispaa, Josephat Ngomale, alisema wafanyabiashara hao wanapaswa kuwa wavumilivu hadi hali itakapo kuwa shwari pia katika nchi jirani ambazo wanazitegemea katika soko la biashara hiyo.

Alisema ni vyema wakati wakiendelea kusubiri hali kurudi kama awali kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona waelekeze nguvu kwenye kukuza soko la ndani ya nchi kwani dagaa na samaki zinazovuliwa katika Ziwa Tanganyika zinahitajika zaidi nchini katika mikoa mbalimbali .

"Nawashauri wafikie mikoa mingi zaidi ikiwamo Mbeya, Arusha na sehemu zingine zenye uhitaji badala ya kuendelea kushindwa kufanyabiashara kwa kutegemea soko la nje," alisema.

Mwalo wa Kibirizi na Katonga kwa mujibu wa taarifa kutoka kitengo cha biashara katika manispaa hiyo kwa mwaka inavua mazao ya uvuvi kiasi cha tani 630 hadi 665.




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, akiangalia sehemu ya mataruma iliyoungwa katika reli ya kisasa ya SGR, sehemu ya Makutupora hadi Morogoro, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, alipokagua maendeleo ya ujenzi wake, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# TUDARCo yaanza kufundisha ubunifu, biashara

**Na Mwandishi wetu**

CHUO Kikuu cha Tumaini Tawi la Dar es Salaam (TUDARCo), kimeendesha kongamano litakalopitia mitaala yake miwili ya ubunifu na ujasiriamali kwa lengo la kupambana na changamoto za ajira na ubunifu kwa wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo.

Vile vile, kupata mitaala ambayo itawakwamua vijana wengi wanaomaliza chuo hicho kuwa wabunifu, kujiajiri na kuajiriwa wanapohitimu.

Mkuu wa chuo hicho, Profesa Burton Mwamila, aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano hilo la siku moja lililowashirikisha wadau mbalimbali katika masuala ya ubunifu na biashara, kwa ajili ya kupitia mkabala mpya wa usanifu na urajamu mpya (re-engineering and rebranding) ili kuboresha huduma zake na muonekano wa chuo.

Awali, Mkurugenzi wa mafunzo na ufundishaji chuoni humo, Dk. Hawa Uiso, alizitaja programu zitakazofundishwa kuwa ni ukuzaji wa ubunifu, ujasiriamali na maendeleo ya biashara pamoja na uhusianishaji wa ujasiriamali na mawazo ya wabunifu.

Naye, Mkurugenzi wa mfuko wa ukuzaji ubunifu wa binadamu (HDIF), Joseph Manirakiza, alisema wameamua kukisaidia chuo hicho baada ya kuona uhitaji na umuhimu wa kuanzisha programu zitakazoweza kufundishwa vyuoni na kuwajengea wasomi kupata elimu, mbinu na uwezo wa kuona fursa na kujiajiri.

Alisema HDIF inashirikiana na taasisi na vyuo mbalimbali katika masuala ya ubunifu, na ndiyo maana imedhamini kongamano hilo.

Manirakiza alitaka utaratibu huo kuwa endelevu ili kusaidia vijana pia kuwalea na kuwaongoza kwenye mawazo yao na ubunifu na kwamba watakuwa tayari kuendelea kushirikiana na kudhamini katika maeneo ya ujasiriamali na ubunifu.

Naye, Mkuu wa Shule ya Biashara chuoni TUDARCo, Dk. Abayo, alisema mitaala hiyo itakapokamilika itaweza kufundishwa kwa chuo kizima kwa programu zote zifundishwazo chuoni hamo na kwa mihula miwili.

# Watafiti watakiwa kutoa matokeo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATAFITI wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameshauriwa kuhakikisha wanawekeza fedha kwa ajili ya kusambaza matokeo ya utafiti kwa walengwa pamoja na kuchangia kutengeneza sera au kuziboresha kwenye maandiko ya miradi yao kwa wafadhili.

Kauli hiyo imetolewa na Mratibu wa Utafiti na machapisho katika Kurugenzi ya Shahada za Uzamili,Utafiti, Uhaulishaji wa teknolojia na ushauri wa kitaalamu kutoka SUA, Profesa Japhet Kashaigili, wakati wa kufunga mradi wa kuwezesha matokeo ya tafiti ili kukuza sera iliyofanyika kwenye kampasi ya Solomon Mhalangu ya Sayansi na Elimu.

Profesa Kashaigili alisema zipo tafiti nyingi na nzuri ambazo zinafanywa na

Watafiti wa SUA, lakini bado mchango wake haujaonekana katika kusaidia utungaji wa na uboreshaji wa sera zilizopo na matokeo yake zinatumika kwenye kuwapatia watafiti shahada na kupanda madaraja.

'' Ukiangalia hata swala la usambazaji wa matokeo ya tafiti zetu mara nyingi tunaweka hela kidogo sana na muda mwingine hatuweki kabisa kwenye baadhi ya miradi ninayoifahamu lakini hili linafanyika bila kujua kuwa uchakataji wa matokeo ya utafiti husika ili kupata sera ni sehemu ya usambazaji wa matokeo kwa walengwa na kutokuweka bajeti maana yeke huna kitu cha kusambaza,'' alisema Profesa Kashaigili.

Alisema kwa sasa kuna ulazima kwa kila mtafiti kujua mbinu muhimu za namna ya kuandika matokeo hayo kwa walengwa wa utafiti kwa kutumia lugha inayoweza kueleweka kirahisi na kufikisha ujumbe kutokana na wengi hawajui kinachofanywa na chuoni hicho.

Hata hivyo, Profesa Kashaigili alipongeza uongozi wa mradi huo kwa kuamua kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Chuoni hapo kuwaeleza malengo ya mradi na matokeo yake na kusaidia hata watafiti wengine kuona kilichofanyika ili kitendo hiko kiigwe na watafiti wengine.

Awali akizungumza kabla ya kufungwa kwa mradi huo Mkuu wa idara ya Mipango, Sera na Utawala ya Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Humanitia, Profesa Fatihia Massawe, alisema ili kuhakikisha kile watafiti wanafanya kinazaa sera wasitegemee utafiti mmoja pekee maana hauwezi kumshawishi mtunga sera kutengeneza sera bali zifanyike nyingi kwenye mitazamo tofauti kama vile Uchumi, Kijamii na hata kiafya.

## Wapinzani wasusia uchaguzi Mkuu Chad

**N'djamena,** CHAD

WAKATI uchaguzi mkuu ulifanyika jana nchini Chad, baadhi ya vyama vya upinzani vimeripotiwa kujitoa katika uchaguzi huo.

Wagombea saba ndio walishiriki kinyang'anyiro hicho, ikiwa ni pamoja na rais anayemaliza muda wake Idriss Déby.

Déby, ambaye yuko madarakani kwa zaidi ya miaka 30 akiwa anatafuta muhula wasita....

Vyama vya upinzani vilivyojiondoa kwenye uchaguzi huo, vililaani vurugu dhidi ya upinzani.

Katika mitaa ya mji mkuu, uchaguzi huo ulizua hisia tofauti.

Wagombea watatu wa upinzani walijiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho mwezi uliopita, yumo mpinzani wa kihistoria wa rais Deby, Saleh Kebzabo.

Kebzabo alitoa wito kwa raia kususia uchaguzi huo na kuungwa mkono na mkosoaji mwingine mkubwa wa rais, Succès Masra.

Mwanasiasa huyo alikataliwa kuwania katika uchaguzi huu, kwa sababu bado ni mchanga kugombea, ingawa aliweza kuhamasisha sehemu kubwa ya vijana ambao wamekuwa wakijaribu kuandamana kila, wiki dhidi ya muhula wa sita wa rais Déby.

Vyama kadhaa vya kiraia, pamoja na mashirika ya haki za binadamu, yameitikia wito wa kususia uchaguzi huo. **RFI**

## Waandamanaji 700 wauawa Myanmar tangu mapinduzi

**Mandalay,** MYANMAR

MLINZI mmoja amejeruhiwa na mlipuko wa bomu jana, katika benki inayomilikiwa na jeshi mjini Mandalay, huku idadi ya vifo vilivyotokana na mapinduzi ya kijeshi kufikia zaidi ya watu 700.

Benki ya Myawaddy ni tawi kubwa kabisa mjini Mandalay, ambalo lililengwa asubuhi ya jana, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya taifa hilo.

Kulionekana idadi kubwa ya maofisa wa usalama kufuatia tukio hilo.

Benki hiyo ni moja kati ya biashara zinazodhibitiwa na jeshi, ambazo zimekabiliwa na shinikizo la kususiwa tangu kutokea mapinduzi, huku wateja wakidai kutoa fedha zao.

Myanmar iliingia katika mkwamo tangu Februari Mosi, mwaka huu, baada ya jeshi kumuondoa madarakani mtawala wa kiraia, Aung San Suu Kyi. **DW**

# UNHCR, Kenya kutafuta suluhu Dadaab, Kakuma

**Geneva,** USWISI

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNCHR), limesema litashirikiana na Kenya kutatua mgogoro wa kambi mbili, Kakuma na Dadaab, zilizotangazwa kufungwa.

Hivi karibuni Kenya ilitangaza nia yake ya kuzifunga kambi hizo zinazowahifadhi wakimbizi na watafuta hifadhi takribani 430,000.

Taarifa ya UNHCR, iliyotolewa hii leo mjini Geneva Uswisi, lilisema litashirikiana na Kenya kuweka mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kupata suluhisho la wakimbizi wanaoishi katika kambi hizo.

**Tunaamini kwamba kupitia hatua mpya za pamoja tutaweka hatua zinazoheshimu haki za wakimbizi.**

UNHCR lilisema, watachukua hatua ikiwamo kuboresha urejeaji wa hiari kwa usalama na hadhi huku wakizingatia vizuizi vya kutembea vinavyohusiana na janga la COVID-19 linaloendelea.

Pia itawekwa mipango mbadala ya wakimbizi wanaotoka katika nchi za Afrika Mashariki kuweza kubaki na kuwapa fursa kwa wakimbizi kujitegemea na kuchangia katika uchumi wa eneo husika.

Kadhalika lilisema itaongezwa kasi ya kutolewa kwa vitambulisho vya kitaifa kwa zaidi ya Wakenya 11,000, ambao awali walitambuliwa kama waliosajiliwa katika hifadhi ya data za wakimbizi na kuendelea kwa mchakato wa uhakiki.

"Tumesikia wasiwasi ulioonyeshwa na serikali ya Kenya na tunatumaini kuwa hatua hizi zitakuwa hatua muhimu katika kuharakisha suluhisho endelevu kwa wale wote wanaohusika." alisema Fathiaa Abdalla, Mwakilishi wa UNHCR, nchini Kenya.

"Tunaamini kwamba kupitia hatua mpya za pamoja tutaweka hatua zinazoheshimu haki za wakimbizi. Tunatarajia kuendelea na mazungumzo na ushirikiano wetu na mamlaka na washirika wa Kenya juu ya jambo hili muhimu." **UN**



Kikosi cha uokoaji kikiwa katika moja ya nyumba ambayo imeathiriwa na tetemeko la ardhi lenye kiwango cha 6.1, lililosababisha vifo vya watu sita, eneo la Majang Tengah kijiji cha Malang, Mashariki mwa Java, nchini Indonesia, juzi. **PICHA: XINHUA**

# Kim Jong-un awaonya raia wake

**Pyongyang,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un (pichani) amewataka raia wa taifa lake, kujitayarisha na janga kubwa, huku makundi ya haki za kibinadamu yakionya kuwa nchi hiyo inakabiliwa na uhaba wa chakula na kuzorota kiuchumi.

Akizungumza katika mkutano, Kim alionekana kulinganisha hali ilivyo sasa hivi na janga kubwa la njaa lililotokea miaka ya 1990.

Korea Kaskazini imefunga mipaka yake kwa sababu ya virusi vya corona.

Pia, ilisitisha uhusiano wake wa kibiashara na China hatua iliyokwamisha uchumi wake.



Aidha nchi hiyo, iliwekewa vikwazo vya kiuchumi kimataifa kwa sababu ya mpango wake wa nyuklia.

Katika hali isiyo ya kawaida ya yenye kukubali kwamba nchi inapitia changamoto, kiogozi huyo, aliwataka maofisa wa chama kukabiliana na kipindi kigumu.

Alitumia neno maarufu kwa maofisa wa Korea Kaskazini, walipozungumzia changamoto ya nchi wakati wa kiangazi kikali miaka ya 1990, pale Muungano wa Usovieti ulipoacha Korea Kaskazini bila usaidizi wa msingi.

Takriban watu milioni tatu inasemekana kuwa walifariki dunia kipindi hicho.

"Sio kawaida kwa kiongozi Kim Jong-un kuzungumzia changamoto anazopitia, lakini anaonekana kuchukua muelekeo mpya," Colin Zwirko, mchambuzi wa Korea Kaskazini wa NK News, alizungumza na Shirika la Habari la Uingereza (BBC).

"Kwa mfano Oktoba mwaka jana, alitoa hotuba na kusema kwamba yeye mwenyewe ameshindwa kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa."

Mapema wiki hii, Kim alionya kuwa nchi hiyo inakabiliwa na hali mbaya zaidi kuwahi kutokea na kutabiri changamoto kadhaa. **BBC**

HABARI MICHEZO

# MBAPPE KUPISHANA NA RONALDO PSG



**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, anaweza kujiunga na Paris Saint-Germain kama Kylian Mbappe ataondoka na kwenda Real Madrid, kwa mujibu wa Tuttosport.

Mbappe amekuwa akihusishwa sana na Real Madrid, huku majaliwa ya Ronaldo kule Juventus yakiwa hayajulikani.

Na sasa ripoti zinaeleza kwamba, Ronaldo ana nafasi kubwa zaidi ya kwenda PSG kama tu Mbappe ataondoka.

Mbappe kwa muda mrefu ameweka roho juu PSG ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwani anaonekana wazi kwamba anataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Hadi sasa nyota huyo mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018, hajakubali kusaini mkataba mpya na PSG.

Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa na Madrid ambao pia wamekuwa wakifukuzia saini za nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland na mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku.

Na sasa ripoti zinaeleza kwamba, kuondoka kwa Mbappe pale PSG maana yake Ronaldo atatua hapo kwenye viunga vya Jiji la Paris.

Ronaldo kwa msimu wa pili mfululizo ameshindwa kuisaidia Juve kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakiwa wanatolewa hatua za mapema, hivyo ana uwezekano mkubwa wa kuondoka pale Turin.

## *Liver waachana rasmi na Konate*

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wameripotiwa kuwa wamewasiliana na RB Leipzig kuwa kwa sasa hawataendelea na dili la uhamisho wa beki wa klabu hiyo, Ibrahima Konate katika dirisha la uhamisho la msimu ujao wa joto.

Wakati kocha Jurgen Klopp akisaka angalau nyongeza ya nguvu kwenye safu yake ya ulinzi ambayo ilikumbwa na shida ya majeruhi, Konate aliaminika kuwapo kwenye rada ya Liverpool pale dirisha la uhamisho litakapofunguliwa.

Kocha Julian Nagelsmann, tayari atakuwa anapunga mkono wa kwaheri kwa Dayot Upamecano baada ya Bayern Munich kukubaliana na dili la mlinzi huyu wa Ufaransa, huku Liverpool na Manchester United wakitajwa kuwa kwenye kinyang'anyiro cha saini ya Konate.

Kwa mujibu wa ripoti, Leipzig waliwasiliana na Liverpool ili kufahamu nia yao ya kumsajili nyota huyo, lakini wamewaambia kuwa hawatarajii kufanya uhamisho wa mchezaji huyo mwenye miaka 21.

Konate pia alisema masuala ya uhamisho wake ni minong'ono tu ambayo yeye mwenyewe amechoka kuisikia.

Konate alinukuliwa na Jarida la France Football, wakati akiwa kwenye majukumu ya kitaifa na kikosi cha vijana cha Ufaransa.



## Conte: Tusishangilie tuendelee kupambana



**MILAN,** Italia

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, amewaambia wachezaji wake kwamba, huu ni wakati wa kufunga mdomo na kupambana kuelekea kwenye ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Inter wapo katika nafasi nzuri sasa ya kulibeba taji hilo, wakiwa wanaongoza ligi kwa tofauti ya pointi 11 kileleni mbele ya AC Milan ambao wapo nafasi ya pili wakiwa na michezo 30.

Na Conte sasa ametaka wachezaji wake kuwa makini kuhakikisha timu yake haipunguzi kasi licha ya kuwa karibu zaidi na ushindi wa taji mapema.

Kwani yeye anaona bado hawajafikia mafanikio ya kuanza kushangilia na badala yake wakaze mwendo kwenye mbio za ubingwa huo na wasiruhusu kupoteza mchezo wowote kati ya iliyobaki.

Conte amekiambia kikosi chake kuwa kwa kuwa taji bado halijapatikana, basi ni kama hawajafanya kitu chochote bado, hadi pale watakapohakikisha wana taji mikononi.

Tangia alipoteuliwa kuwa kocha wa kikosi hicho mwaka 2019, Conte amejitahidi kupalilia jitihada za kikosi hicho, ambacho kimekuwa na ushindani mkubwa na sasa kipo hatua moja karibu na ushindi mkubwa wa kuwang'oa Juventus kwenye utawala wa miaka tisa mfululizo.

HABARI MICHEZO

# Ancelotti amkataa Koulibaly Everton

**LIVERPOOL,** England

EVERTON ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England ambazo zinatajwa kuwania saini ya mlinzi, Kalidou Koulibaly, lakini kocha Carlo Ancelotti, amesema anamchukulia kama "mchezaji mzuri na rafiki mzuri tu", na si sehemu ya mipango yake.

Uhamisho wa fedha nyingi kwenda England kwa beki huyo wa kimataifa wa Senegal umekuwa ukitajwa kwa muda, huku Liverpool na Manchester United wakiripotiwa kuwa wanamuwinda.

Kwa mujibu wa ripoti, 'Tofees' hao walijiunga na harakati hiyo, na Ancelotti anayeiongoza Everton pale Goodson Park amesema ana furaha na walinzi wake wa kati wa sasa ambao anawajumuisha, Michael Kean, Ben Godfrey, Yerry Mina na Mason Holgate.

Ancelotti aliwaambia waandishi wa habari alipoulizwa juu ya mazungumzo ya Koulibaly kuja Everton: "Kusema kweli nina kumbukumbu nyingi nzuri za Koulibaly.

"Alikuwa mchezaji mzuri, mtu mzuri, rafiki mzuri. Lakini ukiona kikosi chetu hapa, tumefunikwa vizuri kwa sababu tuna mabeki wazuri wa kati ambao ni vijana wenye vipaji."

Timu hiyo ya Merseyside iko katika harakati za kupanga mipango yao ya dirisha la msimu wa joto.

Ancelotti amekiri kwamba, anatarajia kuwa katika nafasi ya kuimarisha zaidi safu yake baada ya kuiwezesha Everton kuwania kufuzu michuano ya Ulaya msimu huu.





# GREALISH KUKAA TENA NJE WIKI MBILI

**LONDON,** England

NAHODHA wa Aston Villa, Jack Grealish, anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa wiki nyingine mbili baada ya kutonesha majeraha akiwa mazoezini.

Kiungo huyo amekosa michezo saba ya Ligi Kuu England na mechi za kuwania nafasi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia kutokana na kusumbuliwa na majeraha ya mguu.

Kocha wa Aston Villa, Dean Smith amekiri kwamba Grealish alikuwa mbioni kurejea uwanjani, lakini kwa bahati mbaya ametonesha majeraha yake.

"Hapana, hayuko sawa," alisema Smith, kabla ya mchezo wa Jumamosi dhidi ya Liverpool ambapo walichezea kichapo cha mabao 2-1.

"Mimi na Jack tulikuwa na matumaini kabisa ya kwamba atarejea mapema kidogo lakini kuna shida ambayo imejitokeza hivyo atachelewa kurejea kwa wiki kadhaa."

Grealish ameifungia Aston Villa mabao sita katika Ligi Kuu England msimu huu huku akitoa pasi za mwisho 10, hivyo amehusika kwenye mabao 16.

"Sisi sote, labda tulimsukuma nyuma kidogo haraka sana. Alitaka kurudi, tulitaka arudi na alikuwa na shida kidogo," alisema.

# Liver yamuwania Pedri wa Barcelona

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji, Pedri Lopez kutoka Barcelona, kwa mujibu wa gazeti la Mirror.


Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, ametajwa kwamba ni shabiki na anavutiwa mno na staili ya uchezaji wa nyota huyo wa pale Catalunya.

Liverpool imeijulisha Barcelona juu ya nia yao ya kutaka kumsajili nyota huyo, Lopez na kuiweka 'Blaugrana' katika hali ya hofu ya kumpoteza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kwa sasa, mkataba wake una kifungu cha kuondoka kwa pauni milioni 70 na Liverpool wana nia ya kumsajili kabla ya kifungu hicho kuongezwa.

Barcelona nao wameripotiwa kwamba, wanataka kumwongezea mkataba mchezaji huyo na kwa vyovyote kipengele chake cha kuondoka kitaongezewe dau.

Pedri hadi sasa amecheza mechi 39 katika uzi wa Barcelona akiwa amefunga mabao matatu katika msimu huu wa 2020/2021.



# DON ZA SOKA
## MAGA A ULAYA



# BARCELONA: SI CLASICO YA MWISHO KWA MESSI

**●●● Tuna matumaini ataamua kubaki hapa Camp Nou kucheza nyingi zaidi, sina shaka na...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wana matumaini nahodha wao, Lionel Messi hajacheza El Clasico ya mwisho kwa miamba hao wa LaLiga, amesema Mkurugenzi wa klabu hiyo, Guillermo Amor.

**Messi mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na majaliwa yake pale Barca bado hayajulikani, huku akiwa anahusishwa sana na Paris Saint-Germain na Manchester City.**

Rais wa Barca, Joan Laporta, amebakia ndiye mtu wa kumshawishi Messi kusaini mkataba mpya, ambaye ametumia muda wake wote hapo Camp Nou.

Amor aliulizwa kuhusu majaliwa ya Messi baada ya Barca kufungwa mabao 2-1 kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya Real Madrid, juzi Jumamosi.

"Tumebakiwa na mechi nane kuelekea kufikia malengo yetu ya kutwaa taji la Ligi Kuu Hispania, La Liga.

"Sina shaka kuhusu timu yetu kwamba, tutapambana hadi dakika ya mwisho kabisa ili kulitwaa taji hilo.

"Tuna matumaini kwamba hii sio El Clasico ya mwisho kwake," alisema Amor akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuna matumaini ataamua kubaki hapa Barcelona na kucheza Clasico nyingi zaidi na Barcelona."

Messi alijaribu mara saba kwenye goli la Madrid, ikiwamo kugonga mwamba wakati alipopiga kona ya moja kwa moja kipindi cha kwanza.

Hakuna mchezaji mwingine wa Barcelona ambaye alipiga shuti lolote, na Messi alishindwa kabisa kupenya safu ya ulinzi ya Madrid.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, sasa amecheza Clasico saba kwenye mashindano yote bila kufunga - ukiwa ni ukame wa muda mrefu zaidi dhidi ya Los Blancos hao.

Barca ilikosa nafasi ya kupaa kileleni mwa msimamo wa ligi na sasa kikosi hicho cha kocha, Ronald Koeman kimeachwa nafasi ya tatu kwenye msimamo, kikipitwa pointi moja na Madrid na Atletico Madrid.

## ZISIKUPITE

### KANE KULAZIMISHA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane, 27, atalazimisha kuondoka Tottenham Hotspur kipindi cha majira ya joto kama watashindwa kufuzu michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Athletic)***

### HAALAND KULIPWA ZAIDI

WAKALA Mino Raiola anataka kumfanya straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 20, kuwa mshambuliaji wa kwanza kulipwa pauni milioni moja kwa wiki. Klabu kadhaa zimekuwa zikimuwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway zikiwamo Manchester City na Paris St-Germain. ***(Sunday Mirror)***

### SUAREZ KURUDI LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Luis Suarez, 34, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika Klabu ya Liverpool, miaka saba baada ya nyota huyo wa Uruguay kuondoka pale Anfiled.

### BECKHAM AMTAKA SUAREZ

MMILIKI wa klabu ya Inter Miami ya Marerekan, David Beckham, anawania kumchukua Luis Suarez, 34, ili kukipiga kwenye klabu hiyo msimu ujao. ***(Todofichajes, via Sun on Sunday)***

### RONALDO KWENDA PSG

STRAIKA wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo, 36, anaweza kujiunga na Paris St-Germain kama Kylian Mbappe mwenye miaka 22 ataamua kwenda Real Madrid. ***(Tuttosport, via Mirror)***

### KEAN KURUDI TENA JUVE

STRAIKA wa Everton na Italia, Moise Kean, 21, ambaye anacheza kwa mkopo kule Paris St-Germain, anahusishwa na mpango wa kurudi Juventus. ***(Tuttosport)***

### PEDRI AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji wa Barcelona, Pedri, 18, mwishoni mwa msimu huu. ***(Sunday Mirror)***

### UNITED YAMTAKA NEVES

MANCHESTER United imemuongeza nyota wa Wolverhampton Wanderers, Ruben Neves, 24, katika orodha ya wachezaji inaowania kipindi cha majira ya joto. ***(90min)***

### LINGARD LULU WEST HAM

WEST Ham inataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu, kiungo wa Manchester United, Jesse Lingard, 28, lakini wanakabiliwa na upinzani kutoka kwa Arsenal. Nyota huyo wa England anacheza kwa mkopo kwa 'Wagonga Nyondo' hao wa London. ***(Sunday Star)***

### GORDON AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United na Leeds zimeungana kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kati, Kyron Gordon, 18, kutoka Sheffield United. ***(Sunday)***

HABARI MICHEZO

## KMC FC: Yanga imshukuru refa

**Na Saada Akida**

NYOTA wa KMC FC, David Bryson, amesema Yanga wana kila sababu ya kuwashukuru waamuzi hasa yule wa kati baada ya kuwapa faulo ambayo alidai si sahihi na kupata bao la kusawazisha katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungunza na gazeti hili jijini jana, Bryson aliyefunga bao la KMC FC, alisema walijipanga vizuri, na anaamini faulo ambayo walizawadiwa Yanga haikuwa sahihi kwa sababu beki wao ndiye alifanyiwa madhambi.

"Ni matokeo, tulijipanga kupata matokeo mazuri, lakini pointi moja kwetu si mbaya, ila ninaimani kama si kosa la maamuzi ya waamuzi, basi Yanga wasingepata pointi, kutokana na maandalizi tuliyofanya, " alisema Bryson.

Mchezo huo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi saa 1:00 usiku na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, unaifanya Yanga kufikisha pointi 51 baada ya kushuka dimbani mara 24 huku KMC FC ambayo imecheza mechi 25, ikifikisha alama 36.

## Kiduku amvutia pumzi Dulla Mbabe

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA 'ngumi jiwe' kutoka 'pande' za Morogoro, Twaha Kiduku, amepewa mapumziko ya wiki moja na nusu ili apate nguvu kabla ya kurejea mazoezini kujiandaa kukutana na mpinzani wake Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe', mapema Juni mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana kutoka mkoani Morogoro, Kocha Mkuu wa bondia huyo, Pawa Ilanda, alisema ameamua kumpumzisha Twaha ili mwili wake urejee katika ubora baada ya pambano kali wiki iliyopita kutoa kipigo kwa Tshibangu Kayembe wa DR Congo.

Kocha huyo alisema baada ya kumaliza mapumziko hayo moja kwa moja ataanza kumpa mbinu za kumkabili mpinzani wake huyo ambaye walikuwa wanamhitaji kwa muda mrefu.

# SBL, STARS BEGA KWA BEGA KUFUZU KOMBE LA DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia Bia yake ya Serengeti Lager, ambayo ni mdhamini mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars, imesema itaendelea kuiunga mkono timu hiyo katika jitihada zake za kuwania kufuzu kucheza fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Qatar mwakani.

**Katika michuano ya kuwania kufuzu fainali hizo kubwa zaidi kwa soka duniani, Taifa Stars imepangwa Kundi J pamoja na timu za Taifa za Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Benin pamoja na Madagascar.**

Mkuu wa Kitengo cha Bia wa SBL, Anitha Msangi, aliliambia gazeti hili kuwa kampuni hiyo kama ambavyo imekuwa ikifanya itaendelea kuiunga mkono Taifa Stars na kuongeza kuwa Tanzania inayo nafasi ya kufanya vizuri na kushiriki mashindano hayo ambayo haijawahi kushiriki tangu kuanza kwake mwaka 1930.

"SBL inaendelea kuiunga mkono timu yetu ya taifa kwa sababu tunaamini inaweza kufanya vizuri. Tunafahamu kuwa kufuzu kucheza Kombe la Dunia si jambo rahisi, lakini jitihada za wachezaji pamoja na timu nzima zina kila sababu ya kutufanya tuamini kuwa inawezekana. Tukumbuke kuwa Taifa Stars ilifuzu kushiriki michuano ya mashindano ya Mataifa ya Afrika nchini Misri mwaka 2019 ikiwa ni baada ya miaka 38, hii inaonyesha kuwa inaweza kutupeleka kwenye Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza," alisema Anitha

Anitha alisema Bia ya Serengeti itaendelea kuiunga mkono Taifa Stars na kuwa shabiki namba moja wa timu hiyo huku akiwataka mashabiki na Watanzania kwa ujumla kuendelea kujivunia vya nyumbani ikiwa ni pamoja na timu yao na bia yao ya Serengeti.

"Chapa ya Serengeti ni mdau mkubwa wa michezo hapa nchini na tunaona furaha kuchangia maendeleo ya michezo na tunaahidi kuendelea kuhamasisha na kuchangia maendeleo ya sekta hii ambayo pia huwaleta watu pamoja,' alieleza.

Mwaka jana, Bia ya Serengeti Premium Lager iliingia mkataba wa miaka mitatu na TFF na kuwa mdhamini mkuu wa Taifa Stars kwa makubaliano ya kutoa kiasi cha Sh. bilioni tatu katika kipindi cha mkataba. Mkataba huo unatokana na kumalizika kwa ule wa awali ambao pia ulikuwa ni wa miaka mitatu uliosainiwa mwaka 2017.

Mwaka 2018, SBL kupitia bia yake pendwa ya Serengeti Lite pia iliingia mkataba wa miaka mitatu na Shirikisho la Soka Tanzania na kuwa mdhamini mkuu wa Ligi ya Wanawake ikiwa ni mara ya kwanza kwa ligi hiyo kupata mdhamini tangu ianze na kuifanya SBL kuwa mdhamini wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini.

**SISIMUA...**



Mtangazaji wa East Africa TV, Kelvin Lyimo maarufu kama 'Kevoo' (Kulia), akifurahia picha ya pamoja na 'kuselfika' na wanafunzi wa shule za sekondari jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa Kampeni ya 'Sisimua Maisha na Fanta' hivi karibuni iliyofanyika Dar es Salaam. Kampeni hiyo imeziduliwa na Coca-Cola Tanzania ikilenga kuhamasisha burudani, rangi na michezo mbalimbali inayopendwa na vijana. **MPIGAPICHA WETU**

# *Beki Simba aitabiria kutinga fainali CAF*

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa Simba, Said Koko, amesema kikosi hicho kinaweza kabisa kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwani kina uwezo mkubwa wa kupambana na timu yoyote ile Afrika kwa sasa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Koko beki wa kati aliyeichezea timu hiyo mwanzoni mwa mwaka 2000 hadi 2007, alisema kama iliweza kucheza dhidi ya Al Ahly ambao ni mabingwa wa Afrika nyumbani kwao kwa utulivu kiasi kwamba wenyeji walitamani mpira umalizike huku wakiwa na ushindi finyu tu wa bao 1-0, basi inaweza kupambana na timu yoyote ile iwe nyumbani au ugenini.

Simba itacheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na timu moja wapo kati ya MC Alger na CR Belouzdad zote za Algeria, au Kaizer Cheifs ya Afrika Kusini.

"Nimeiangalia Simba mechi zake zote ilizocheza na hata ile ya Al Ahly, wako vizuri, ina wachezaji wazuri ambao wanaweza kukupa matokeo sehemu yoyote ile. Na kwenye michuano hii ili ufanye vizuri na kusonga mbele ni lazima uwe na wachezaji ambao wanaweza kucheza nyumbani na ugenini kwa uwezo sawa," alisema Koko raia wa Burundi.

Alimsifu mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji na kusema kuwa kwa muda mfupi tu tangu aingie, Simba imekuwa na mafanikio makubwa ndani na nje ya uwanja, kitu ambacho kuna klabu zingine kubwa huchukua muda mrefu.

"Ubora wa Simba wote unachangiwa na pesa. Mpira siku zote ni pesa. Mo amekuja kuwekeza, amesajili wachezaji wazuri ambao ndiyo wanaoleta furaha kwa Wanasimba tena kwa muda mfupi tu. Unajua unaweza kuwekeza ukakaa hata zaidi ya miaka mitano, lakini miaka mitatu tu hii tangu kuingia imekuwa ni bora ndani ya uwanja na nje, kwa hiyo watu wajifunze hili la kuwekeza kwenye soka," alisema.

# Michezo

Jumatatu Aprili 12, 2021

Nipashe




Mbappe kupishana na Ronaldo PSG UKURASA 20

PAGUMU LEO...



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, akijaribu bila mafanikio kukwamisha mpira wa faulo ndogo nyavuni kwenye mechi ya LaLiga iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi na Real Madrid kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Simba kwa Waarabu wa Algeria robo fainali CAF

## ● ● ● Mguu pande pia kwa Kaizer Chief Aprili 30, Gomes asema kikosi chake kipo tayari kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, akisema kuwa kwa sasa anaelekeza akili yake kwenye Ligi Kuu Bara na Kombe la FA na wapo tayari kwa mshindani yeyote watakayepangiwa kwenye droo ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatimaye sasa wapinzani wao wamejulikana rasmi kuwa ni Waarabu wa Algeria ama droo pia inaweza kuangukia kwa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

**Simba imefuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa kuongoza Kundi A kwa pointi 13, lililokuwa likizijumuisha Al Ahly ya Misri iliyomaliza nafasi ya pili na pointi 11ikifuatiwa na AS Vita ya DR Congo pointi saba na Al- Merrikh ya Sudan ikiburuza mkia na alama zake mbili.**

Hata hivyo, mabingwa hao wa Tanzania Bara, baada ya mechi yao ya mwisho walivyolala kwa bao 1-0 Ijumaa iliyopita ugenini dhidi ya Al Ahly, walikuwa wakisubiri kukamilika kwa mechi za hatua ya makundi juzi, Jumamosi ili kujua timu tatu ambazo moja inaweza kukutana nayo robo fainali.

Kwa mujibu wa kanuni za michuano hiyo, vinara kutoka kila kundi watakutana na timu zilizoshika nafasi ya pili, lakini si kutoka kundi lake, hivyo Simba haiwezi kukutana na Al Ahly waliyokuwa kundi moja na badala yake sasa itakutana na moja kati ya timu tatu kutoka Kundi B, C na D ambazo ni CR Belouizdad na MC Alger za Algeria, ama Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Kwa upande wa Al Ahly nayo inasubiri Aprili 30, mwaka huu wakati wa upangaji wa droo ya robo fainali kujua kama itakutana na mshindi yupi kati ya walioongoza Kundi B, C na D, ambao ni Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Wydad Casablanca ya Morocco anayoichezea Mtanzania Simon Msuva ama ES Tunis ya Tunisia.

Mabingwa wa kila kundi pia watakuwa na faida ya kuanzia ugenini katika mechi hizo za mtoano ambazo zitachezwa nyumbani na ugenini na mshindi wa jumla kutinga robo fainali ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Hata hivyo, wakati huu Simba ikirejea sasa katika Ligi Kuu Bara, Gomes amesema vita sasa wanaihamishia katika mbio za ubingwa pamoja na kutetea Kombe la FA.

Amesema timu zote nane zilizotinga hatua ya robo fainali ni bora barani Afrika, hivyo wanarejea kwenye ligi lakini pia kujipanga kwa hatua inayofuata ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kauli hiyo iliungwa mkono na beki kisiki wa kati wa timu hiyo, Muivory Coast Pascal Wawa, ambaye amesema kuwa licha ya kushiriki mashindano ya kimataifa bado wana hesabu za kufanya vizuri kwenye ligi ya ndani.

"Hii michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika imekuwa ni migumu sana, lakini kadiri tunavyopiga hatua ndiyo matarajio na malengo yetu yanazidi kuwa makubwa maana tumefikia kwenda kucheza robo fainali na malengo tufike nusu fainali, hivyo sasa tunareja Ligi Kuu kwanza," alisema.

Simba ambayo ipo nafasi ya tatu na kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 46 baada ya kucheza mechi 20, Jumatano itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Mtibwa Sugar kabla ya kusafiri kwenda kuivaa Mwadui FC Jumamosi mkoani Shinyanga.

Yanga ndiyo inayoongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 51 baada ya kucheza mechi 24 ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 47 zilizotokana na kushuka dimbani mara 25.

# Mwambusi aanika sababu sare Yanga SC

**Na Saada Akida**

TAMBO na majigambo zinaendelea kutawala kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wanaendelea vizuri na mazoezi, ushindani unaoonekana unaonyesha kila mmoja ana kiu ya kupata matokeo chanya katika mchezo huo.

Hafidh alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo kwa sababu wanahitaji kuibuka mabingwa wa msimu huu.

"Tumejipanga na kujiimarisha, tumerekebisha upungufu uliyokuwapo kwa ajili ya kurejea na kasi mpya, tunajua mechi zote ni ngumu, hivyo hatutabweteka," meneja huyo alisema.

Naye Ofisa Uhusiano wa KMC, Christina Mwangala, alisema timu yake itaingia uwanjani ikiwa na lengo la kusaka ushindi ili kujiimarisha katika msimamo na hatimaye kutimiza malengo waliyonayo.

Mwangala alisema wamejiandaa kukabiliana na ushindani kwa sababu kila timu imedhamiria kuondoka na alama tatu muhimu katika mchezo huo huku KMC inaamini hakuna kitakachoshindikana.

"Tunakwenda kwenye mchezo ambao kimsingi hautakuwa mwepesi kutokana na aina ya timu ambayo tunakutana nayo, ni nzuri, wanafanya vizuri, lakini pia wanaongoza ligi, hivyo mchezo utakuwa mgumu, pamoja na yote bado KMC FC tunasema kwamba tunakwenda kupambanania alama tatu na tunaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mchezo wetu," alisema Mwangala.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza wenyeji KMC walifungwa mabao 2-1, goli pekee la kikosi hicho cha Manispaa ya Kinondi lilifungwa na Hassan Kabunda dakika ya 23.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >